BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,010,689,585/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



UKURASA 5

**RAIS** Samia atoa ya moyoni miaka 30 ya vyama vingi Tanzania




Ijumaa Julai 1, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580993
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


Nipashe
HUKU ADA IKIFUTWA:
Hivi ndivyo ilivyo michango shuleni
Askari polisi apigwa ... akijihami
Meli kubwa yatia nanga na shehena ya mbolea

# Serikali: Marufuku michango shuleni

**Fomu** za kujiunga sharti idhini ya RAS... *Ukurasa 2*



Rais na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Samia Suluhu Hassan, akimvalisha cheo kipya cha Jenerali Jacob John Mkunda, kabla ya kumwapisha kuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi nchini (CDF), Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Mkuu wa Majeshi alivyokula kiapo, mstaafu Mabeyo kupewa jukumu

UKURASA 3

UKURASA WA 4

## BWENI LA WANAFUNZI LAUNGUA MOTO

WANAFUNZI 76 wa Shule ya Sekondari ya Wavulana Bwiru iliyoko wilayani Ilemela mkoani Mwanza, wamepoteza vifaa vyao vya masomo baada ya bweni lao kuwaka moto. Ajali hiyo ya moto ikitokea majira ya saa 3:36 usiku wa kuamkia jana, huku vyombo vya ulinzi na usala...

UKURASA WA 4

## MEYA MOSHI APATIKANA, CCM YALIA NA MAKUNDI

ZUBERY Kidumo, Diwani wa Njoro (CCM) ameibuka kidedea kwa kura 27 (asilimia 96.4) katika kinyang'anyiro cha Umeya wa Manispaa ya Moshi, akimshinda mpinzani wake, Frank Kagoma (CHADEMA) aliyepata kura moja (asilimia 3.6). Uchaguzi huo umefanyika ...

UKURASA WA 8

## MBUNGE ABOOD ATOA MISAADA YA MAMILIONI



MBUNGE wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood (CCM) ametoa msaada wa magari ya kubebea wagonjwa mawili yenye...

# Mawakili wa CHADEMA, kina Mdee hapatoshi mahakamani

UKURASA 2




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, akibadilishana hati na Balozi wa Marekani hapa nchini, Donald Wright, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kutiliana saini makubaliano kati ya benki hiyo na mashirika ya Kimarekani ya USAID na DFC ya kuwezesha mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 100, zitakazoiwezesha CRDB kutanua wigo wa uwezeshaji wa mikopo kwa wanawake na vijana sambamba na kutoa mikopo katika sekta za elimu, afya na zisizo rasmi nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**MICHEZO** WAZIRI MKUU AIPONGEZA YANGA UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akisoma hotuba ya kuahirisha mkutano wa saba wa Bunge la 12, jijini Dodoma, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yapiga marufuku michango kwenye shule

**Na Salome Kitomari,**
DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameiagiza Ofisi ya Rais -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ishirikiane na sekretarieti za mikoa na halmashauri zote kufuatilia matumizi na upatikanaji wa taarifa za fedha za elimumsingi bila ada kuhakikisha wanafunzi hawatozwi michango kiholela.

Vilevile, amezitaka taasisi hizo zihakikishe kuanzia sasa maelezo ya kujiunga na shule za umma yanahakikiwa na kupewa idhini na Katibu Tawala wa Mkoa husika kwa kushirikiana na maofisa elimu wa maeneo husika.

Aliagiza hayo jana wakati akitoa hoja ya kuahirisha Mkutano wa Saba wa Bunge la 12 bungeni jijini Dodoma, akibainisha kuwa asilimia 10 ya fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Utoaji Elimumsingi Bila Ada, hutumika kugharamia huduma za umeme, maji na ulinzi.

"Pamoja na utekelezaji wa mpango huu, waheshimiwa wabunge wamelalamikia kuwapo utitiri wa michango shuleni. Serikali kupitia waraka wa elimu namba tano wa mwaka 2015 na waraka wa elimu namba sita wa mwaka 2015, imetoa maelekezo bayana kuhusu utekelezaji wa elimumsingi bila ada," alisema.

Waziri Mkuu alisema maelekezo hayo ni pamoja na matumizi ya fedha za utawala ambazo hutolewa Hazina na kupelekwa moja kwa moja katika akaunti za shule za msingi na sekondari nchini kwa ajili ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia, ukarabati, uendeshaji wa mitihani ya ndani na utawala.

Waziri Mkuu alitumia fursa hiyo kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa maono na dhamira yake kutekeleza kwa vitendo maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020 kuhusu serikali kutoa elimumsingi bila ada kwa ngazi ya shule za msingi na sekondari kwa lengo la kuimarisha mazingira ya utoaji wa elimu, mahudhurio na ufaulu.

**MAANDALIZI SENSA**

Majaliwa pia alisema maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 yanaendelea vizuri na yamefikia asilimia 87, hivyo akawaomba wabunge hususan wanaporejea kwenye maeneo yao ya uwakilishi, waendelee kuhamasisha wananchi kushiriki kwenye sensa hiyo muhimu.

"Nitoe wito kwa Watanzania wote kujiandaa kuhesabiwa ikiwa ni pamoja na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa makarani wa sensa na viongozi kwenye maeneo wanayoishi. Zoezi hilo limepangwa kufanyika nchini kote Agosti 23, 2022," alikumbusha.

Waziri Mkuu alisema sensa imetanguliwa na Operesheni ya Anwani za Makazi ambayo utekelezaji wake umefikia asilimia 95 na serikali imefanikiwa kukusanya taarifa na kutoa anwani za makazi zaidi ya milioni 12.

Sambamba na mafanikio hayo, Waziri Mkuu alizielekeza taasisi zote zenye dhamana ya masuala ya ardhi na makazi zihakikishe zinakuja na mikakati thabiti ya kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi iliyoainishwa wakati wa utekelezaji wa operesheni anwani za makazi.

Waziri Mkuu alisema mbali na kuwa na mikakati ya kutatua migogoro ya ardhi, pia taasisi hizo zitoe miongozo ya namna bora ya kushughulikia kero za Watanzania kuishi katika maeneo yasiyoruhusiwa kisheria ili kuhakikisha wananchi wote wananufaika na fursa zitokanazo na zoezi hilo.

Waziri Mkuu pia alielekeza uhakiki wa majina ya mitaa katika vibao uendelee kufanyika ili kujiridhisha kuhusu usahihi wake.


PPTL

TAARIFA KWA UMMA



Michael Ole Musa

Hii ni kutaarifu Umma kwamba mwenye picha hapo Juu amejiuzulu na si mfanyakazi tena wa **Pee Pee Tanzania Ltd** kuanzia tarehe **20/06/2022**

Tunaomba kutangazia umma kwamba Kampuni ya Pee Pee Tanzania Ltd haitahusika na miamala itakayoagizwa au shughuli yoyote itakayofanywa na mtajwa kwa jina la Kampuni. Muamala au uwakilishi wowote kwa niaba ya kampuni utafanywa kupitia **0784249114.** au Email: **marketing@pptl.biz**, **sales@pptl.biz**

**Utawala.**

116926701


# Mawakili wa CHADEMA, kina Mdee hapatoshi mahakamani

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Masjala Kuu mnamo Julai 6, 2022 inatarajia kutoa uamuzi wa maombi ya Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee na wenzake 18 kama watapewa kibali cha kuwasilisha mapitio ya kimahakama wakipinga kuvuliwa uanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Tarehe hiyo ilipangwa jana na Jaji Mustapha Ismail baada ya kusikiliza hoja za mawakili wa CHADEMA, mawakili wa Mdee na wenzake na baada ya kupokea maoni ya kisheria kutoka kwa Wakili wa Serikali.

Wakati wakiwasilisha hoja zao, Wakili wa Waleta Maombi (Mdee na wenzake), Ipilinga Panya, alidai wamewasilisha ombi hilo wakiwa na hoja tano ambazo zitachambuliwa na jopo la mawakili wanne, ikiwamo ya kwamba walifungua maombi hayo ndani ya muda wa kisheria.

Alidai hoja nyingine ni kuonyesha kuna jambo linalobishaniwa, kuonyesha maslahi ya waleta maombi, CHADEMA ni chombo cha umma na kama walitafuta haki zao ndani ya chama hicho.

Wakili Panya alidai maombi hayo yamefunguliwa kwa wakati kwa kuwa yalitakiwa yaombwe ndani ya miezi sita tangu kutolewa kwa uamuzi unaolalamikiwa na hivyo, Mdee na wenzake wamefungua maombi yao ndani ya muda.

Alidai waleta maombi wote ni wabunge wa viti maalum walioteuliwa na Bodi ya Chama hicho mwaka 2020/2025, hivyo uamuzi wa kuwafukuza uanachama bila kufuata utaratibu wa kuwasikiliza unagusa maslahi yao binafsi.

Wakili Panya alidai Mdee na wenzake wana maslahi mapana katika jambo hilo, wameathirika na uamuzi wa bodi hiyo kupitia uamuzi wa Baraza Kuu la chama hicho wa Mei 11, 2022 uliowafukuza uanachama.

Akizungumzia kama kuna jambo linalobishaniwa, Wakili Aliko Mwamanenge alidai waleta maombi wote hawakusikilizwa na kusababisha uamuzi wa Kamati Kuu ya CHADEMA wa Novemba 27, 2020 na uamuzi wa Mei 11,2022 wa Baraza hilo na suala hilo halikupingwa na chama hicho.

Wakili Mwamanenge alidai viapo vyote vya waleta maombi 19 vinaonyesha kuna msukumo wa nguvu kutoka kwa CHADEMA, kikimtaka Spika wa Bunge achukue hatua ya kuitaarifu NEC ili viti wanavyoshikilia waleta maombi wote, viachwe wazi.

Wakili Ebson Kilatu alizungumzia hoja ya kama Baraza la Wadhamini la CHADEMA wakati linachukua uamuzi wa kuwavua uanachama Mdee na wenzake lilikuwa ni kama chombo cha umma kwa mujibu wa majukumu ya vyama vya siasa, akidai kinatakiwa kizingatie majukumu ya utoaji haki wakati kinawafukuza wanachama wake, kuzingatia demokrasia utawala bora na hata kutobagua jinsia.

Akijibu hoja hizo, Wakili Peter Kibatala alidai hawabishi hoja kwamba Mdee na wenzake wana maslahi mapana ila kigezo cha mgogoro hakiangaliwi juu juu, bali lazima kuwapo ushahidi mahakamani chini ya kiapo ili mahakama ichunguze na hawajauwasilisha.

"Mahakama haiwezi kuwapa nafuu wanazoomba waleta maombi kwa sababu wamewasilisha maombi hayo nje ya muda wa miezi sita tangu walipofukuzwa uanachama Novemba 27, 2020," alidai.

Wakili Kibatala alidai hawabishi waleta maombi kwenda mahakamani, lakini njia waliyotumia ilikuwa siyo sahihi kwa kuwa walichelewesha hoja zao kwa kuiomba mahakama kwa njia ya mapitio.

Alidai watu 28 hawawezi kubadili uamuzi wa wajumbe 437, waleta maombi walikuwa wanaijua Katiba ya CHADEMA kwamba wajumbe wa Kamati Kuu wanaingia katika Baraza Kuu, hivyo haikuwahi kuleta shida na haiwezi kuwa hoja ya msingi.

Wakili Kibatala alidai CHADEMA siyo chama cha umma na hakifanyi kazi za umma kama ilivyoelezwa na waleta maombi.

Wakati akitoa maoni yao, Wakili wa Serikali, Stanley Kalokola, alidai kwamba hawajawasilisha kiapo kinzani kwa hiyo hawapingi hoja za kwenye viapo lakini pia kwa maoni yao, Mdee na wenzake walifungua maombi hayo ndani ya muda.

Mdee na wenzake walifungua kesi hiyo dhidi ya Baraza la Wadhamini la Chadema, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

## HABARI KITAIFA

# Kaya 290 zajiandikisha kuhama kwa hiari Ngorongoro

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

JUMLA ya kaya 293 zenye watu 1.497 zimejiandikisha kuhama kwa hiari ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) kwenda Kijiji cha Msomera wilayani Handeni mkoani Tanga.

Vilevile jana kaya 25 zenye jumla ya watu 115 zilisafiri kwa hiari kuelekea Msomera kuendelea na maisha yao huku jumla ya nyumba 103 zikikamilika kujengwa na nyingine 400 ujenzi unaendelea pamoja na maandalizi ya mashamba na huduma za kijamii kwa wananchi hao.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alibainisha hayo bungeni jijini hapo jana wakati akitoa hoja ya kuahirisha Mkutano wa Saba wa Bunge la 12.

Alisema katika kuhakikisha wakazi wanaohama wanakuwa na maisha bora zaidi, serikali ilitoa motisha kwa kila kaya inayoondoka inapewa fidia ya nyumba iliyokuwa inaishi.

Alisema kaya zinapatiwa nyumba zenye vyumba vitatu kwenye eneo la ekari 2.5, godoro, tochi na ndoo; shamba lenye ukubwa wa ekari tano na watakabidhiwa hati za kumiliki ardhi kwa ajili ya eneo la nyumba na shamba.

Waziri Mkuu alibainisha kuwa kila kaya inapewa fedha za kutosha kwa ajili ya kuanzia maisha kwenye makazi mapya; na mahindi magunia mawili kwa kipindi cha miezi mitatu kwa ajili ya kujikimu katika kipindi cha mpito wakati wakazi wakijiandaa kwa maandalizi ya kilimo.

"Utaratibu huu ni maalum kwa Ngorongoro pekee. Ninawapongeza wananchi wote walioridhia kuhama kwa hiari. Juni 23, mwaka huu, nilitembelea Ngorongoro na nilipata fursa ya kuwaaga wananchi wanaohama kwa hiari kutoka hifadhi ya Ngorongoro kwenda Msomera ambao waliishukuru serikali," alisema.

Waziri Mkuu alisema serikali imeendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu fursa za eneo la Msomera lililoko Handeni kiuchumi na kijamii kupitia vikao vingi na wananchi wa eneo la Ngorongoro wakiwamo viongozi wa mila (Laigwanak), madiwani, watendaji wa kata na vijiji, wawakilishi wa kinamama, vijana na wadau wengine. "Hadi sasa, kumekuwa na mafanikio makubwa katika kusimamia utekelezaji, serikali imeendelea kuhamasisha na kuandikisha zile kaya ambazo zipo tayari kuhama kwa hiari," alisema.

**LOLIONDO**

Waziri Mkuu alisema uwekaji wa vigingi katika eneo la Pori Tengefu la Loliondo umekamilika kwa asilimia 100 na kwamba hautoathiri maendeleo ya wakazi wa eneo la vijiji 14 vinavyopakana na eneo hilo. Alisema hakutakuwapo na kijiji kitakachofutwa na hakuna miundombinu itakayoondolewa kwa kuwa ndani ya eneo la kilometa za mraba 1,500 hakuna miundombinu yoyote.

"Serikali imesimamia kwa umakini mkubwa zoezi la uwekaji vigingi kwenye eneo la kilometa za mraba 1,500 ambalo ni muhimu kwa ikolojia ya Hifadhi ya Serengeti na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

"Serikali imeendelea kushirikiana na wananchi wa Loliondo katika kuboresha malisho ya mifugo, uchimbaji wa visima vya maji, ujenzi wa majosho pamoja na miundombinu ya kunyweshea mifugo kwenye eneo la kilometa za mraba 2,500," alisema.

Waziri Mkuu alielekeza Wizara ya Maliasili na Utalii kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na wadau wengine kuhakikisha Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya Mwaka 1999 inatumika ipasavyo kutenga na kuweka mipaka ya vijiji.

"Serikali kwa kuzingatia matakwa ya wananchi, hasa maeneo ya malisho kwenye vijiji 14 vilivyoko karibu na Pori Tengefu la Poloreti itaweka utaratibu utakaopangwa kwa pamoja baada ya kukamilisha utambuzi wa mifugo kwenye vijiji husika," alisema.

Pori Tengefu la Loliondo lina kilomita za mraba 4,000 na limekuwa likitumiwa na wananchi kuendesha shughuli za kibinadamu kama vile kilimo, ulishaji wa mifugo na makazi pamoja na shughuli za uhifadhi na utalii.

Alisema matumizi yasiyo rafiki yamekuwa chanzo cha kuharibika kwa mfumo wa ikolojia wa pori hilo muhimu kwa ajili ya kulinda Mfumo Ikolojia ya Serengeti, ikiwamo maeneo ya mazalia, makazi na mapito ya makundi makubwa ya nyumbu wahamao.

Kwa mujibu wa Majaliwa, sababu kubwa ya kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa Serengeti ni kuhifadhi mzunguko wa nyumbu ambao kwa kiasi kikubwa uko upande wa Tanzania na umuhimu wake kama urithi wa dunia.

Eneo la Ngorongoro lilianzishwa mwaka mwaka 1959 kukiwa na watu takriban 8,000 na mifugo 161,000, lakini hadi sasa idadi ya watu inakadiriwa kuwa takribani 110,000 na mifugo 1,000,000.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Barua Pepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Mtumba,**
**S.L.P. 2888,**
**40470DODOMA,**
**30 - 06 - 2022**

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kutaarifu umma kuwa siku ya Alhamisi **Jumapili tarehe 03–07–2022** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd.** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-es-Salaam Port** kuelekea **Rufiji**, gari hizo zenye namba za usajili:

**T 468 DYG / T 837 DJB**
**T 464 DYG / T 887 DJB**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 22 Upana - mita 4.60 Kimo - mita 4.60**

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam**, **Pwani** hadi Rufiji kupitia **Kibiti**, gari zitasafiri muda wa mchana tu (**Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni**)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

116927501


# Mkuu wa Majeshi alivyokula kiapo

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewaapisha viongozi wapya wa juu jeshini; Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Tanzania, Jenerali Jacob Mkunda na Mnadhimu Mkuu, Luteni Jenerali Salum Othman.

Halfa hiyo fupi iliyofanyika jana Ikulu jijini Dar es Salaam, ilianza kwa wakuu hao wapya kuvuliwa vyeo vya zamani na kuvalishwa vipya, Jenerali Mkunda akitoka cheo cha Meja Jenerali na kuwa jenerali huku Othman akitoka cheo cha Meja Jenerali na kuwa Luteni Jenerali.

Baada ya tukio hilo, viongozi hao walirudi tena kwa ajili ya kuapishwa na Amiri Jeshi Mkuu, Rais Samia Suluhu Hassan, Jenerali Mkunda akiapishwa rasmi kuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Tanzania.

Baada ya kiapo hicho, Jenerali Mkunda alikwenda kupokea salamu ya Mkuu wa Majeshi kwenye gadi maalum iliyoandaliwa kwa ajili hiyo kisha kurudi katika kiti chake.

Ikafuata zamu ya Luteni Jenerali Othman ambaye alikula kiapo kwa Amiri Jeshi Mkuu kuwa Mnadhimu Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi wa Wananchi Tanzania.

Akizungumza baada ya kuwaapisha viongozi wao, Rais Samia aliwapongeza kwa hatua hiyo, akiwataka kuendeleza pale walipoachia viongozi waliowatangulia na kwamba mambo mengine walitarajia kuzungumza baada ya hafla hiyo.

"Mkaanze pale Jenerali Mabeyo alipoishia, mnajua kwenye jeshi hakuna mtu kuingia na yake kama tulivyo kwenye serikali. Ukifika mwenzio alipoachia unaanza hapo unakwenda mbele, maelezo zaidi tutazungumza inbox," alisema Rais.

Pia alimpongeza Jenerali Mabeyo kwa kumaliza kazi yake nzuri aliyoitumikia kwa miaka 40 kwa uadilifu na jitihada kubwa.

"Umefanya kazi yako kwa uadilifu mkubwa, umetumikia cheo chako kwa jitihada kubwa na leo unamaliza na kukabidhi kwa wengine. Tunakushukuru sana na tunakupongeza sana kwa sababu siyo kazi rahisi," alisema Rais Samia.

Hata hivyo, Rais Samia alisema serikali itampangia kiongozi huyo majukumu mengine kwa kuwa bado ana nguvu.

"Tutaendelea kukupa majukumu uweze kutusaidia, nadhani jioni ya leo (jana) Katibu Mkuu Kiongozi (Balozi Hassan Katanga) utasikia kwenye bomba tayari ameshakupangia kazi ya kufanya," alisema Rais.

Hafla hiyo ya kusisimua ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali na kijeshi akiwamo Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Akson na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Stegomena Tax.


**IN LOVING MEMORY OF**
**THE LATE CRISPIN S.E. MWANYIKA**



**14th Feb 1946 - 02nd July 1999**

*"Our beloved was called home to be with the good Lord. But the life of the dead is placed in the heart of the living, to live in the hearts of those we love is never to die"*

**Life is meant to be a celebration, today we as family, relatives and friends are celebrating your life which was a blessing, remembering the memories we shared and treasuring each moment. Because someone we love is in heaven, there's a little bit of heaven in our hearts.**

**THERE WILL BE A REQUIEM MASS AT ST NICHOLAUS ROMAN CATHOLIC CHURCH, MTONGANI- KUNDUCHI BEACH ON SUNDAY 03.07.2022 AT 9.00AM.**

**Eternal rest grant unto him, O Lord, and let perpetual light shine upon him. May his soul and the souls of all the faithful departed, through the Mercy of God, Rest in peace.**

**AMEN.**
**Joshua 1:9**

216926502

# Bweni la wanafunzi laungua

**Rose Jacob,** MWANZA

WANAFUNZI 76 wa Shule ya Sekondari ya Wavulana Bwiru iliyoko wilayani Ilemela mkoani Mwanza, wamepoteza vifaa vyao vya masomo baada ya bweni lao kuwaka moto.

Ajali hiyo ya moto ikitokea majira ya saa 3:36 usiku wa kuamkia jana, huku vyombo vya ulinzi na usalama mkoani hapo vikisema wanafunzi wote wako salama.

Kufuatia ajali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, amewatoa hofu wanafunzi hao, akisema kuwa mkoa wake utahakikisha wote wanapata vifaa vyote vya shule vilivyoteketezwa na moto ili waendelee na masomo yao.

"Ninaomba msihofu, vyombo vya ulinzi vipo hapa vinafanya kazi jengo hili lililoshika moto limepasuka, presha ilikuwa kali kule juu, hivyo muwe makini halifai, lipo chini ya ulinzi.

"Kwanza lazima uchunguzi ufanyike ili tujiridhishe chanzo cha moto ni nini na baada ya hapo tutalibomoa, kikubwa muwe watulivu, sisi tutasimamia kuhakikisha vifaa vyote muhimu vyenu wanafunzi 76 mnavipata na mnarudi katika maisha yenu ya kawaida," alisema Gabriel.

Akizungumzia tukio hilo kwa niaba ya wanafunzi wa shule hiyo, Jamal Iddy alisema kuwa wakati wakiwa darasani wakijisomea majira ya usiku, walisikia kengele ya dharura na walivyotoka walikuta moto unawaka katika bweni lao.

"Mpaka sasa hatujajua chanzo cha moto ni nini wala nani kafanya hivyo, maana tulikuwa darasani tunasoma, tulipokea taarifa baada ya kengele kugongwa na moto ulikuwa umeishaanza kuwaka, ilikuwa kwenye saa tatu kuelekea saa nne usiku," alisimulia Iddy.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mwanza, Ambwene Mwakibete, alisema hakuna kifo kilichotokea na kwamba baada ya kupata taarifa ya tukio hilo, walichukua hatua za haraka ili kudhibiti moto huo kupunguza madhara zaidi.

Mwakibete alisema wanafanya uchunguzi ili kujua chanzo cha moto huo, athari kwa wanafunzi na jengo hilo.

"Shule hii ina mabweni 11 lakini moja ndiyo lililoathirika na moto huu, tulifanikiwa kuuzima ili usienea maeneo mengine na ulitokea majira ya saa 3 na dakika 36 usiku wa Juni 29.

"Hakuna madhara kwa binadamu kwani hakuna mwanafunzi yoyote aliyepata madhara wala kuathiriwa na moto huo kwa sababu bahati nzuri wanafunzi muda huo walikuwa macho na hawakuwa kwenye bweni hilo, walikuwa darasani katika mazingira ya kujisomea," alisema Mwakibete.




Ofisa Masoko wa Kampuni ya Gf Trucks & Equipment's Ltd, Lukolo Juma (kushoto), akielezea ubora wa gari mpya ya FAW-CA1073, wakati wa uzinduzi wa gari hiyo kwa ajili ya wakulima na wajasiriamari wadogo, kwenye maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Menejimenti Nishati yakagua maendeleo Bwawa la Nyerere

**Na Zuena Msuya,** PWANI

WAJUMBE wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati wamefanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) na kubainisha kuridhishwa na kasi ya ujenzi wa mradi kulingana na fedha alizolipwa mkandarasi.

Akizungumza kwa niaba ya Mwenyekiti wa Menejimenti ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara, Mkurugenzi wa Idara ya Sera na Mipango, Petro Lyatuu, amesema lengo la ziara hiyo ni kufuatilia na kukagua utekelezaji wa mradi huo ambao ni mkubwa na wenye maslahi makubwa kwa Taifa.

Lyatuu alisema jana kuwa Wizara ya Nishati ni msimamizi mkuu wa utekelezaji wa mradi huo ambapo pamoja na kumwezesha kifedha mkandarasi anayetekeleza mradi huo, wizara ina jukumu kubwa la kufuatilia kwa karibu na kutathmini kama malipo ya fedha yanaendana na kazi iliyofanyika.

Alifafanua kuwa mpaka sasa serikali imekwishamlipa mkandarasi zaidi ya Sh. trilioni nne, sawa na asilimia 61 ya fedha anazotakiwa kulipwa kwa kazi iliyokwishafanyika.

"Wizara ni msimamizi mkuu wa mradi wa JNHPP na wakuu wa idara na vitengo katika wizara wana dhamana ya kufuatilia, kukagua, kutathmini na kushauri kuhusu utekelezaji wa mradi huu ili malengo ya mradi yafikiwe kama ilivyokusudiwa," alisema Lyatuu.

Wajumbe waliofanya ziara hiyo ni Wakuu wa Idara na Vitengo kutoka Idara ya Utawala na Rasilimali Watu, Idara ya Sera na Mipango, Idara ya Umeme na Nishati Jadidifu, Idara ya Petroli na Gesi, Kitengo cha Ununuzi, Kitengo cha Sheria, Kitengo cha Uhasibu, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, Kitengo cha TEHAMA, Kitengo cha Mawasiliano Serikalini na Kitengo cha Mazingira.

Akizungumza kwa niaba ya Wakuu wa Idara na Vitengo vya wizara, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Ziana Mlawa, alisema wizara imeweka utaratibu kwa wakuu wa idara na vitengo kutembelea miradi inayotekelezwa na wizara ili kuona na kufahamu kwa ukaribu kazi wanazozifanya kwa maandishi wawapo ofisini.

Mlawa aliweka wazi kuwa ziara hizo zinawapa nafasi ya kufahamu kero wanazokumbana nazo watumishi wanapotekeleza majukumu yao katika maeneo mengine hasa katika miradi mbalimbali inayotekelezwa mbali na maeneo ya ofisi.

Wajumbe hao wametembelea na kukagua maeneo mbalimbali ya mradi wa JNHPP ambapo walikagua maendeleo ya ujenzi wa tuta kuu la bwawa, kituo cha kuchochea umeme, nyumba ya kuendeshea mitambo ya kuzalisha umeme na kingo za bwawa (Saddle Dam).

Pia walikagua maendeleo ya ujenzi wa daraja la kudumu, barabara, njia ya kupeleka maji kwenye mitambo ya kuzalisha umeme, nyumba za watumishi pamoja na eneo la ufungaji wa mitambo.

Vilevile, walizuru katika eneo litakalojengwa kituo cha kupoza umeme utakozalishwa katika mradi wa JNHPP na kusambazwa katika maeneo mbalimbali nchini kilichoko Chalinze mkoani Pwani pamoja na njia ya kusafirisha umeme mkubwa wa Kv 400 utakaozalishwa katika mradi huo.

## Meya Moshi apatikana, CCM yalia na makundi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

ZUBERY Kidumo, Diwani wa Njoro (CCM) ameibuka kidedea kwa kura 27 (asilimia 96.4) katika kinyang'anyiro cha Umeya wa Manispaa ya Moshi, akimshinda mpinzani wake, Frank Kagoma (CHADEMA) aliyepata kura moja (asilimia 3.6).

Uchaguzi huo umefanyika kutokana na kuondolewa madarakani kwa aliyekuwa meya wa manispaa hiyo baada ya kukumbwa na tuhuma mbalimbali.

Akitangaza matokeo hayo, Mkurugenzi wa Manispaa ya Moshi, Rashid Gembe, alisema mjini hapo jana kuwa kura zilizopigwa ni 28, mgombea wa CCM akipigiwa kura 27 huku mgombea wa CHADEMA akipata kura moja.

"Wajumbe halali ni 28, jumla ya kura zilizopigwa ni 28 na hakuna kura iliyoharibika," alisema.

Mwenyekiti CCM Moshi Mjini, Alhaji Omari Shamba, alionya kuwa madiwani hao wasipobadilika na kuimarisha umoja, ushirikiano na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo, mwaka 2025 hawatapata fursa ya kurudi katika baraza hilo kama madiwani.

"Ni kweli kulikuwa na makundi mawili ila kwa sasa yamekwisha, leo (jana) siyo siku ya furaha sana, maana kilichotokea siyo jambo la kufurahisha kwa CCM Moshi Mjini, haijatupendeza sisi kumtoa meya wetu na kumweka mwingine kabla ya muda kuisha kwa sababu ambazo hazikufurahisha.

"Siku tukimwapisha Juma Raibu hapa, tuliongea na leo Zubery ninarudia, uache tabia za kitoto za ujana kama unazo na uache makundi yasiyofaa huku ukitambua kwanzia leo umekuwa baba wa Manispaa ya Moshi, utulie uwatumikie wananchi. Ukienda kinyume, litakufika lililomfika Juma Raibu," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema hawawezi kuwa na madiwani wasiopendana na wasio na umoja katika manispaa hiyo, huku akiwataka madiwani kuhakikisha wanakusanya kodi ili wananchi wapate maisha bora.

Mwenyekiti wa CHADEMA Manispaa ya Moshi, Legius Nchimbi, alimtaka meya mpya huyo kutumia nafasi aliyopata kuwaunganisha madiwani wote wa baraza hilo huku akimpongeza mgombea wa chama hicho kwa demokrasia aliyotumia.

Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Abas Kayanda, alimtaka meya huyo kuhakikisha anamtegemea Mungu kwa kila kitu atakachokifanya, huku akiahidi kutoa ushirikiano wa hali na mali katika kuhakikisha maendeleo yanapatikana katika manispaa hiyo.

Meya Kidumo aliahidi watahakikisha miradi yote ya maendeleo itakayokuja katika manispaa hiyo, inasimamiwa vyema, inapitiwa vyema na kwa wakati kama ilani ya chama chao inavyoelekeza.

"Ninaahidi ushirikiano, kuwa tayari kujifunza, kuwa msikivu wakati wote, kuonyeka, kushauriwa, kuleta ushirikiano kwa baraza la madiwani pamoja na kuhakikisha miradi yote ya maendeleo inafanyika kwa wakati na kukabidhiwa kwa watu sahihi," aliahidi.

Nafasi hiyo ilikuwa wazi kuanzia Aprili 11, 2022 baada ya aliyekuwa Meya wa Manispaa hiyo, Juma Raibu, kung'olewa katika wadhifa huo na madiwani wakimtuhumu kwa mambo mbalimbali, yakiwamo ya kimaadili.

## Apendekeza kufutwa kifungu kinachoingilia uhuru wa mhariri

**Na Mary Geofrey**

MAKAMU Mwenyekiti wa MISA-TAN, Wakili James Marenga, amependekeza kufutwa kwa kifungu cha 7 (2) (b) cha Sheria ya Huduma za Habari kwa sababu kinaingilia uhuru wa mhariri wa kutoa au kuchapisha habari.

Wakili Marenga, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumzia Sheria ya Huduma za Habari na marekebisho yanayotakiwa kufanyika.

Akifafanua alisema, kifungu hicho kinapoka mamlaka ya mhariri katika kuamua habari gani ya kuchapishwa.

"Kifungu cha 7 (2) (b) (iv) cha Sheria ya Huduma za Habari, kinatoa maelekezo kwa vyombo vya habari binafsi kuchapisha habari zenye umuhimu kwa taifa kwa maelekezo ya serikali.

Kinaingilia uhuru wa uhariri na hasa kwenye vyombo vya habari vya binafsi. Kifungu hiki kidogo hakiwezi kufanyiwa marekebisho, tunapendekeza kifutwe," alisema Wakili Marenga. Alisema mapendekezo yanakusudia kuwezesha maamuzi ya kihariri kuzingatia vigezo vya taaluma bila kuathiriwa na maamrisho yasiyo ya kitaaluma na kwamba uhuru wa uhariri (editorial independence) utalindwa.

Kadhalika, alisema kifungu cha 7 (3), (a), (b), (c), (f), (g), (h), (i) na (j) vya sheria hiyo, vinatoa udhibiti wa aina fulani ya habari ama maudhui.

"Mamlaka hii ya kisheria inatoa mwanya kwa serikali kudhibiti taarifa zinazotolewa na vyombo binafsi vya habari.


"Kifungu hiki na vifungu vyake vidogo vinakiuka uhuru wa kujieleza bila ya kuwa na sababu za msingi. Hii pia ni kwa mujibu wa maamuzi ya Mahakama ya Haki ya Afrika ya Mashariki (EACJ)," alisema Wakili Marenga.

Alisema, tunapendekeza kifungu hiki na vifungu vyake vidogo vifutwe kama ilivyoamuliwa na Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki (EACJ).

Naye Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri (TEF), Deodatus Balile, alisema wameungana kwa pamoja kuhakikisha wanaweka mazingira rafiki kwa wanahabari kufanya kazi zao.

"Kuna sheria nyingi zilizowekwa na kulenga waandishi au kushambulia tasnia, kwa kuwa tumeungana kwa pamoja kuhakikisha sheria hizo zinaondolewa makali yanayoumiza wanahabari.

"Ni bahati nzuri sasa serikali nayo imeliona hili, mwelekeo wetu na matumaini lakini tunapaswa kuendelea pamoja mpaka tunafikia lengo," alisisitiza Balile.



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na Chama Cha Mapinduzi (CCM) siku walipokutana na kufanya mazungumzo. **PICHA: MAKTABA**

## MIAKA 30 YA VYAMA VINGI:

# Changamoto na mustakabali kusonga mbele

**Na Samia Suluhu Hassan**

LEO Tanzania inatimiza miaka 30 tangu turejee rasmi katika siasa za mfumo wa vyama vingi. Katika kipindi hicho, taifa letu limepitia katika kipindi cha furaha, majonzi, misukusuko na changamoto zote wakati taifa linapoanza njia mpya. Jambo hili si jepesi kwa sababu nyakati hizo hazikuwa rahisi duniani kote.

Miaka ambayo Tanzania ilirejea katika mfumo huo ilikuwa miaka migumu. Miaka ya mwanzoni ya 1990, ndiyo ilishuhudia changamoto kama vile kuanguka kwa iliyokuwa Urusi, vita vya wenyewe kwa wenyewe barani Afrika, mauaji ya kimbari na migogoro mingi ya kisiasa na kiuchumi katika nchi zinazoendelea kama yetu.

Lakini Watanzania walipita katika wakati wote huo wakiwa wamoja na tumeendeleza utamaduni huo miaka 30 baadaye. Napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza wote na ni matumaini yangu makubwa kwamba viongozi watakaokuja miaka 50 hadi 100 baadaye, wataendelea kuongoza nchi iliyo moja na wananchi wasiobaguana na kupigana hata kama wanapingana kuhusu namna ya kuendesha nchi yao.

Ni vizuri kuzungumza kuhusu namna tulivyoingia katika mfumo huu. Rais Ali Hassan Mwinyi aliunda Tume ya Jaji Francis Nyalali iliyokuja na majibu kwamba ni asilimia 20 tu ya Watanzania ndiyo walitaka mfumo wa vyama vingi. Ni busara ya Mzee Mwinyi na viongozi wenzake wa wakati huo walioamua kusikiliza wachache. Kama wazee wetu wangesubiri mpaka asilimia 80 itake vyama vingi ndiyo tukubali, pengine leo tusingekuwa tulipo. Hili ni miongoni mwa mafunzo makubwa kwa wanasiasa wa kizazi changu na watakaokuja baadaye. Kwenye jambo la maslahi ya nchi, maarifa na busara ndiyo muhimu kuliko namba.

Kutoka kuwa na chama kimoja cha siasa - Chama Cha Mapinduzi (CCM), sasa tuna vyama vilivyosajiliwa takribani 20. Badala ya kusikia sauti moja na wakati mwingine tukisema "Zidumu Fikra za Mwenyekiti", sasa Watanzania wanasikia kuhusu fikra za sauti tofauti. Kwa bahati nzuri, hata Mwenyekiti Mao alipata kusema "Acha maua 100 yamee kwa pamoja".

Kipekee kabisa, nitumie nafasi hii kuwapongeza wote waliofanikisha safari hii. Viongozi wa CCM na Serikali walioona umuhimu wa kuruhusu vyama vingi kabla vita na vurugu havijatulazimisha na wanaharakati na wasomi waliokuwa wakisaidia kutuonyesha kuwa tunatakiwa kuingia katika mfumo wa vyama vingi.

Hata hivyo, yatakuwa makosa makubwa kama tutaona kuwa kazi ile imemalizika. Ninaamini, sasa tunapita katika mazingira yale yale magumu yaliyokuwapo wakati tunaanza mfumo wa vyama vingi. Kuna vita katika maeneo mbalimbali duniani ikiwamo kwenye nchi zilizoendelea, mfumo wa kidemokrasia wa kiliberali unapitia katika changamoto na nchi kubwa zinapambana kuwania kutawala dunia. Ni changamoto ambazo viongozi wa kizazi chetu wanatakiwa kuzivuka kama walivyofanya watangulizi wangu.

Ndiyo sababu kwenye uongozi wangu ninaamini katika kile kinachojulikana kama 4R - ikiwa ni ufupisho wa maneno manne ya lugha ya Kiingereza; Reconcilation (Maridhiano), Resiliency (Ustahamilivu), Reforms (Mabadiliko) na Rebuilding (Kujenga Upya).

### MARIDHIANO

Katika tamthilia maarufu ya karne ya 19 ya Iolanthe, waandishi Gilbert na Sullivan walieleza jambo moja kuhusu taifa la Marekani wakati huo; " Kila anayezaliwa ni ama mtoto mhafidhina au mtoto mliberali". Mimi siamini kwenye misimamo ya namna hii. Kwamba mwanadamu, awe mwanasiasa, kiongozi au mwananchi wa kawaida, kuwa na msimamo usiobadilika kuhusu mambo yenye maslahi kwa taifa. Msimamo au hali fulani inaweza kueleweka au kukubalika wakati fulani lakini si wakati wote. Si wakati wakati wote ni wa kupongezana na si wakati wote ni wa kupingana.

Kwenye kujenga Tanzania bora ninatamani kujenga jamii yenye maridhiano na maelewano. Ninatamani kujenga umoja pasipo kujali tofauti zetu za kisiasa, kidini, kikabila na nyingine zote. Hili litawezekana kwa kujenga jamii inayopata haki sawa mbele ya sheria, isiyobaguana na inayotoa fursa sawa za kiuchumi kwa wote. Ninaamini maridhiano hayawezi kupatikana penye ubaguzi na pale ambapo kuna wanaokosa fursa na haki zao za kiuchumi na kiraia.

### USTAHAMILIVU

Kama alivyopata kuasa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, ujenzi wa taifa si lelemama. Tanzania hii haiwezi kusonga mbele kama sisi wananchi na viongozi wenu tutakuwa legelege kulinda yaliyo yetu. Wahenga walisema Umoja ni Nguvu na namna pekee ya kupambana na changamoto zote zinazoikumba dunia kwa sasa ni kwetu sisi kufanya hivyo kwa Umoja na Mshikamano.

Huko tuendako tutatikiswa na kuyumbishwa. Iwe kiuchumi, kimazingira, kijamii na kisiasa lakini ni lazima tujenge ustahamilivu. Hii ni kwa sababu hakuna nchi nyingine zaidi ya hii na hapa ndiyo kwetu. Nilitiwa nguvu sana na namna Watanzania walivyopokea tukio la Royal Tour kwa uzalendo wa kipekee.

### MABADILIKO

Kuna msemo mmoja maarufu kwamba kitu pekee cha uhakika kwa mwanadamu ni mabadiliko. Nimedhamiria kwamba kwenye kuenzi miaka yetu ya demokrasia ya vyama vingi, serikali yangu itajitahidi kufanya mabadiliko katika mifumo ya kisiasa, kiuchumi na katika sheria zetu za uchaguzi. Lengo ni kwamba Tanzania yetu iende na wakati na kama ilivyokuwa wakati mwingine, tujue mapema ni wakati gani wa kufanya jambo hata kama si watu wanaliunga au hawaliungi mkono kwa wakati husika.

Mabadiliko katika sheria zetu za uchaguzi yataleta ushindani wa haki na kuwapa watu fursa ya kuwachagua wawatakao kuwaongoza. Kwenye uchumi, mabadiliko yatakuwa na lengo la kutoa fursa zaidi kwa watu wengi zaidi kunufaika kiuchumi badala ya wachache.

### KUJENGA UPYA

Ninafahamu kwamba wananchi hawali maridhiano, ustahamilivu wala mabadiliko. Mwisho wa siku kama walivyofanya watangulizi wangu wengine kwenye karne hii; Benjamin Mkapa, Jakaya Kikwete na John Magufuli, lengo kuu linatakiwa kuwa ukuaji wa uchumi wetu. Uchumi utakaoongeza ajira kwa vijana wetu na utakaofungua fursa kwa makundi yote ya kijamii yaliyo nchini.

Tayari tunaendeleza miradi mikubwa ya miundombinu na mengine kwenye sekta ya madini na nishati. Juhudi zilizofanywa kupitia kampeni ya Royal Tour zina lengo la kuzimua sekta muhimu ya utalii iliyoathiriwa sana na ugonjwa wa Covid- 19. Katika kilimo tunakwenda kufanya mabadiliko mengine makubwa ili sekta hiyo muhimu ianze kuwa na mchango inaostahili kwenye uchumi wetu.

Ninaamini kwamba kwa jitihada zetu za R nne, tutaweza kutimiza malengo ya kuwa na mfumo wa vyama vingi vya siasa. Lengo kuu halikuwa kuwa na vyama vingi vya siasa bali lengo lilikuwa kujenga jamii yenye uzalendo, maridhiano, ustahamilivu na yenye uchumi unaokua kwa wote na endelevu. Hii ndiyo namna bora ya kuendeleza ndoto za wale waliopigania vyama vingi.

**Kazi na Iendelee.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mwaka 2022/23 upoze ugumu huu wa maisha

**BUNGE** limemalizika na sasa bajeti ya serikali ya mwaka 2022/23 inaanza kufanyakazi kuanzia leo Julai Mosi. Hongera kwa mwaka mpya wa fedha wa serikali.

Ni muda ambao Watanzania wanaamini kuna mabadiliko yanayokuja kwenye sekta mbalimbali kama maji, tiba, miundombinu hasa barabara na madaraja, vyote fedha zake zimepitishwa bungeni na sasa kinachosubiriwa ni utekelezaji.

Wakati bajeti inapopitishwa na mwaka mpya wa serikali ukianza Watanzania wengi wanalalamikia gharama ya juu ya maisha inayowaadhibu mamilioni mijini na vijijini.

Bei za vyakula kama mchele, sembe, unga wa ngano na mafuta ziko juu mno. Sembe inaelekea kufikia Shilingi 2,000 wakati mchele wa daraja la chini au wenye chenga nyingi unakaribia Shilingi 2,000.

Lakini pia, wakati mwaka mpya wa fedha unaanza bidhaa zingine za nyumbani zinazotumiwa na mamilioni ya Watanzania zimekuwa zikiongezeka bei kwa kasi tangu kuanza mwaka huu kutokana na athari za mfumuko wa bei.

Bidhaa hizi ni pamoja na sabuni za kufulia za vipande, na sasa mche umefikia zaidi ya Shilingi 4,000, wakati mafuta ya kula lita moja inaanzia Shilingi 7,000.

Wakati mwingine mafuta hayo hayana viwango na kuna madai kuwa chanzo chake hakifahamiki na kuna uwezekano wa kutumia mafuta yaliyochakachuliwa.

Mafuta ya taa yanayotumiwa zaidi vijijini na wakazi wa mijini wasio na uwezo wa kumudu gesi hasa kuandaa vyakula kwa ajili ya watoto wanaokwenda shuleni alfajiri au wale wanaotumia jiko la 'Mchina' ni ghali mno kuna maeneo mengine lita moja imefikia Shilingi 5,000.

Ikumbukwe mafuta haya hayapo kwenye vituo vya mafuta ni mitaani na madukani kusiko na bei elekezi, hiyo si habari njema kwa wanaotegemea nishati hii.

Tatizo jingine ni bei kubwa mno ya vifaa vya ujenzi kuanzia mbao, mabati, rangi,marumaru, vioo , mabamba ya vyuma (bars) nondo, mchanga na kokoto pia.

Lakini, kwa wajasiriamali mathalani wafuga kuku, vyakula viko juu mno na kuongeza ugumu kwa wajasiriamali wafugaji ambao kwa upande mwingine wanashindwa kupandisha bei ya nyama na mayai.

Orodha ni ndefu lakini miongoni mwa mambo yanayozungumzwa karibu kila mahali ni gharama kubwa ya maisha. Wakati mwaka wa fedha ukianza kinachojiri ni malalamiko ya kiwango kikubwa cha ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana na kukosekana mbinu za kujiajiri.

Tunaiomba serikali kuendelea kufikiria tena namna ya kupunguza bei za vyakula vikuu hasa mahindi, ngano, mchele na maharage.

Tunaiomba serikali iangalie namna bora ya kuondoa au kupunguza kodi na tozo zinazotozwa kwenye mashine za kuzalisha unga.

Pengine kuna vibali kutoka mamlaka mbalimbali kuanzia za udhibiti wa ubora, afya za wafanyakazi, ubora wa bidhaa, kodi za halmashauri hadi serikali kuu ili kupunguza gharama za sembe.


Tunaomba pia iangalie kodi zinazotozwa kwenye mali ghafi za kuzalisha sabuni na hata vyakula vya mifugo kama kuku ili kupunguza gharama kubwa za ufugaji na hata za kuzalisha vifaranga ambavyo pengine viatamizi (incubators) ni kubwa na kupandisha bei za vifaranga ambayo sasa inakaribia 3,000.

Kwa serikali hakishindikani kitu tunaiomba kuangalia maeneo mengine yanayopandisha gharama za maisha ikiwamo nishati hasa gesi, umeme na mkaa.

Inaweza kuleta urahisi kwa kuweka ruzuku kwenye gesi ya mitungini ili ipungue bei, pia kuondoa kodi kwenye vifaa vya umeme vya kupikia yakiwamo majiko ili kusaidia changamoto za ughali wa nishati zinazoongeza pia gharama za maisha.

Heri kwa mwaka mpya wa fedha wa serikali , tunaombea mafanikio kwa kila lililopangwa bungeni Dodoma.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wana Dar mpo? Kujichunga muhimu tumeambiwa UVIKO-19 bado tunao

Na Sabato Kasika

**MCHANGANUO** wa idadi ya watu waliothibitika kuambukizwa ugonjwa wa UVIKO-19, unaonyesha kuwa mkoa wa Dar es Salaam ni kinara kwa kuwa na watu wenye ugonjwa huo kuliko mikoa mingine nchini.

Walioambukizwa ugonjwa huo Dar es Salaam ni 130, Arusha 10, Mwanza watano, Kilimanjaro, Kitavi, Morogoro, Simiyu na Mbeya, mmoja mmoja, Shinyanga wanne, Mtwara watatu, Dodoma na Mara wawili wawili.

Ni takwimu za Mei 5 hadi Juni 3, mwaka huu zilizotolewa hivi karibuni na Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichwale, katika tamko lake kwa umma juu ya mwenendo wa ugonjwa huo.

Anasema, Mei 5 hadi Juni 3 mwaka huu, watatu waliopata chanjo ni 775, 680, huku Wizara ya Afya ikiendelea kusisitiza watu kujitokeza kupata chanjo na chukua tahadhari zote ikiwamo kuvaa barakoa.

Aidha, anasema visa vipya vya maambukizi ya UVIKO-19 vimeendelea kurikodiwa nchini katika kipindi cha Mei 22 hadi Juni 3, mwaka huu, vikionyesha kuendelea kuongezeka kwa maambukizi ya ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa Dk. Sichwale, kuna visa vipya 161 vya maambukizi mapya ya UVIKO-19 katika kipindi hicho cha Mei hadi Juni mwaka huu, ikilinganishwa na visa 68 vilivyorekodiwa kwa kipindi cha Aprili 2 hadi Mei 4 mwaka huu.

Ninadhani kwamba, hali hiyo inatosha kutuonyesha kuwa kuna haja ya watu kuhamasika na kampeni ya chanjo, ili wajitokeze kwa wingi kwenda katika vituo vya kutolea chanjo, kwa ajili ya kulinda afya zao.

Serikali na wadau wa afya wamekuwa wakifanya kampeni za kuhamasisha chanjo maeneo mbalimbali nchini, lakini bado jamii imekuwa na kigugumizi kujitokeza kwa wingi kupata chanjo.

Ugumu huo unaweza kuwa chanzo cha kuendelea kuwapo UVIKO-19 nchini, hivyo ninadhani kuna haja kwa kila Mtanzania kutafakari na kuchukua sahihi za kuhakikisha analinda afya yake dhidi ya ugonjwa huo.

> **Serikali na wadau wa afya wamekuwa wakifanya kampeni za kuhamasisha chanjo maeneo mbalimbali nchini, lakini bado jamii imekuwa na kigugumizi kujitokeza kwa wingi kupata chanjo.**

Kwa wakazi wa Dar es Salaam, ni vyema wakachukua hatua sahihi za kupata chanjo haraka iwezekanavyo, ili kupunguza idadi ya maambukizi ya ugonjwa huo, ambayo yanaonyesha kuwa juu kuliko mikoa mingine nchini.

Wakati watu wakisuasua kupata chanjo, Katibu Mkuu Msaidizi na Mratibu Mkuu wa Kimataifa wa mapambano dhidi ya UVIKO-19, wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Dk. Ted Chaiban, anatarajia kuja nchini kuhamasisha chanjo.

Mratibu huyo anatarajia kutua nchini wiki ijayo kwa ziara ya siku nne yenye lengo la kuhamasisha Watanzania kupata chanjo ya UKIKO-19, pamoja na mambo mengine yanayohusiana na afya.

Huenda ujio huo unatokana na hatua zilizochukuliwa na Wizara ya Afya hivi karibuni, za kuzindua kampeni iitwayo Global Vax Initiative yenye lengo la kuhamasisha jamii kupata chanjo na kufuatilia wale ambao hawajaikamilisha.

Kwa hali hiyo, ambayo sasa inawaleta wakubwa kuja kuhamasisha chanjo, ninadhani ipo haja kwa kila Mtanzania kuchukua hatua zote zinazoelekezwa na Wizara ya Afya ili kuwa salama dhidi ya UVIKO-19.

Ukweli ni kama jamii imejihalalisha kuchukua hatua zinazoelekezwa na wizara husika, kwani sasa ni jambo la kawaida kwa wakazi wa Dar es Salaam kutozingatia maelekezo ya kujikinga na ugonjwa.

Watu hawavai barakoa, hawanawi maji tiririka wala kutumia vitakasa mikono, wanarundikana katika masoko, vituo vya mabasi wanajazana katika vyombo vya usafiri bila kujali kwamba hiyo ni hatari kwa afya zao.

Enyi wakazi wa Dar es Salaam, kujichunga ni muhimu, kwani takwimu za Wizara ya Afya zinaonyesha kuwa mkoa wenu unaongoza kwa idadi kubwa ya watu waliothibitika kuwa na ugonjwa huo.

HABARI KITAIFA




Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani), kuhusu ushiriki wa benki hiyo kwenye Maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yanayoendelea katika viwanja vya Jk Nyerere Barabara ya Kilwa. Kushoto ni Meneja wa NMB Tawi la Temeke Sabasaba, Kidawa Masoud. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tuhuma za rushwa zaponza wakuu idara

**Na Ibrahim Yassin,** SONGWE

MKUU wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, amemwagiza Katibu Tawala Mkoa huo kuwasimamisha kazi watumishi wanne wa idara za mipango, ununuzi, mhandisi na mwekahazina ili kupisha uchunguzi wa tuhuma zinazowakabili ikiwapo rushwa.

Watumishi hao ni wakuu wa idara katika Halmashauri ya Wilaya ya Songwe ambao ni Ofisa Mipango na Fedha Fransica Nzota, Mwekehazina Oscar Msalikwa, Ofisa Ununuzi Nuru Mkali na Mkuu wa Idara ya Ujenzi, Hilda Semsela.

Mgumba alitoa agizo hilo juzi baada ya kupokea malalamiko ya wananchi katika Kata ya Ngwala kuwa baadhi ya maofisa wilayani humo hudai rushwa kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mmoja wa wananchi hao ambaye hakujitambulisha jina, alidai wamekuwa hawapati huduma stahiki wanapofika kwenye ofisi hizo. Alidai kuwa kama hauna fedha za kutoa rushwa ni ngumu kupatiwa huduma, akimwomba kiongozi huyo wa mkoa kufanya ziara za kushtukiza katika halmashauri hiyo ili abaini 'madudu' zaidi kwa watumishi hao ambao wanakwamisha utekelezaji wa shughuli za serikali na wananchi.

Mbunge wao, Philipo Mulugo, alimweleza Mkuu wa Mkoa kupitia mkutano huo wa hadhara kuwa amekuwa akitoa huduma kwa wananchi wakiwamo watendaji wanaotoka vijijini kufuata huduma za kiofisi wilayani kutopatikana kutokana na ubabaishaji wa wakuu hao wa idara.

Alisema hata katika utekelezaji wa fedha za mfuko wa jimbo imekuwa ni shida kwake kwa kuwa kitengo cha fedha na mipango kina shida.

Alifafanua kuwa katika ziara zake vijijini, amekuwa akikumbwa na malalamiko mengi juu ya watendaji hao ambao wamekuwa wakikwamisha shughuli za kiutendaji. Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Abraham Sambila, alikiri kuwapo kwa malalamiko hayo.

Baada ya maelezo hayo, Mgumba alimwagiza Katibu Tawala mkoani humo, Misaile Musa, kuunda kamati ya uchunguzi wa tuhuma hizo wakati watuhumiwa wakiwa nje ya ofisi, pia aliiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupamba na Rushwa (TAKUKURU) kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo wilayani humo kubaini uhalisia zaidi.

Mgumba pia alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Cesilia Kavishe, kuwasimamisha na kuwachukulia hatua watumishi wote wote waliotajwa kuwa na tuhuma za rushwa. Ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe ya kukagua miradi ya maendeleo na kusikiliza kero za wananchi ilifikia tamati jana katika Wilaya ya Songwe, akibaini upungufu kadhaa kwa baadhi ya watendaji ambao aliagiza wawajibishwe.

# SUMAJKT yajikita katika kilimo kikubwa

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT) limesema wakati likiadhimisha miaka 41 ya kuanzishwa kwake, limejikita zaidi katika shughuli za kilimo kikubwa na sasa limefungua mashamba makubwa ya umwagiliaji yenye vifaa vya kisasa.

Katika maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa, maarufu Sabasaba, Kaimu Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa SUMAJKT, Kanali Shija Lupi, alisema Dar es Salaam juzi kuwa wamefungua maonyesho yao ikiwa ni sehemu ya kusherehekea miaka 41 tangu shirika hilo lianzishwe Julai Mosi, 1981.

Alisema SUMAJKT ina kampuni zake tangu na wapo katika maonyesho hayo kwa lengo la kuonyesha bidhaa mbalimbali katika sekta za kilimo, ufugaji, viwanda, biashara na huduma.

"Katika sekta ya kilimo, SUMAJKT imejikita katika kilimo kikubwa kulingana na maelekezo ya serikali, tumefungua mashamba makubwa ya umwagiliaji kama la Mgeta lenye vifaa vya kisasa lililoko Morogoro.

"Katika sera ya taifa upande wa chakula, tunasaidia usalama wa chakula. Katika miaka yetu 41, tumeleta mradi mkubwa wa SUMAJKT Agri-Mashinery unaouza matrekta na zana za kilimo ili kuhakikisha mkulima anazalisha chakula kwa kutumia bidhaa hizo za kisasa zaidi badala ya jembe la mkono," alifafanua.

Kuhusu masoko ya kikanda, Kanali Lupi alisema kwa sasa mchele unaozalishwa Morogoro, unauzwa kwenye masoko ya nje mikoa ya kusini na Kanda ya Ziwa.

Kuhusu mikakati yao ya sasa, Kanali Lupi alisema tayari wamepanua mashamba na badala ya kutegemea mvua, wanatumia kilimo cha umwagiliaji.

"Katika sekta ya ujenzi, shirika limekuwa likifanya shughuli zake hasa ujenzi wa kimkakati wa baadhi ya shughuli inazopewa na serikali, tumefanya vizuri kwa kuisaidia serikali kutekeleza sera zake, mfano ujenzi wa ukuta wa Mirerani," alisema.

Kwa upande wa viwanda, alisema kuwa katika miaka 41 wameweza kuvifungua vipya na vile walivyoanza navyo wamevikarabati na kuzalisha bidhaa zenye ubora zikiwamo za samani.

Pia alisema wanazalisha bidhaa ya maji ijulikanayo kama Uhuru Peak ambayo imetoa ajira nyingi.

Kanali Lupi alisema katika sekta ya ufugaji, wana kampuni ijulikanayo kama SUMAPONICS ambayo hujishughulisha na ufugaji wa samaki kwa kutumia mitambo na bidhaa za plastiki ambapo vitu vyote hivyo vimesaidia pato la mtu mmoja mmoja kwa sababu wamekuwa na mafunzo ya namna ya kuwafuga na kuwakuza.

"Miaka 41 SUMAJKT imefanya mambo makubwa hasa ya kuinua kipato cha Mtanzania mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya SUMAJKT, Meja Jenerali (mstaafu) Farah Mohamed, alisema shirika hilo lina miradi mikubwa ambayo inajitegemea na imeendelea kukua na kuongeza ufanisi na tija katika utekelezaji wake.

Alisema lengo ni kuona nchi inakuwa na miradi ambayo ni sehemu ya kukuza uchumi wa nchi na kutatua matatizo kwenye jamii, ikiwamo ya ajira.

# Wadau selimundu wahoji bajeti yao

**Na Mary Geofrey**

MENEJA wa Kituo cha Selimundu Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Malula Nkanyemka, ameiomba serikali ieleze kiasi cha fedha kilichotenga kwa ajili ya mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

Amesema kuwa pamoja na serikali kuingiza ugonjwa huo kwenye mpango wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza, kuna umuhimu wa kujua bajeti inayotengwa ili wafahamu kama inatosha.

Malula alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari wakati akitoa shukrani kwa serikali kwa ajili ya tuzo aliyopatiwa Profesa Julie Makani wa MUHAS kwa kutambua mchango wake katika kuimarisha huduma ya afya kwa ugonjwa huo nchini.

"Tunaomba tujue gharama ambazo serikali imetenga kwa ajili ya wagonjwa wa selimundu ili tunapokwenda kwenye mashirika mbalimbali, tuwaeleze takwimu za kiasi kilichotengwa kwa kazi hii na upatikanaji wa hizo taarifa ni muhimu sana," alisema Malula.

Alisema licha ya jitihada kubwa zinazofanywa na wadau na serikali katika kupambana na ugonjwa huo, bado wananchi wana mwamko mdogo wa kujua afya zao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi Zinazojihusisha na Selimundu (TANSCDA), Dk. Degratius Soka, alitaja mafanikio manne yaliyopatikana kutokana na juhudi mbalimbali walizofanya, yakijumuisha kuwa na kliniki za watoto wenye selimundu ambazo zinapatikana katika hospitali mbalimbali nchini.

Alisema serikali imeingiza ugonjwa huo katika mpango mkakati wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza, pia kumeanzishwa shahada ya uzamili nchini na kusaidia kupatikana kwa madaktari bingwa wa damu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

"Eneo lingine ni utafiti, umefanyika utafiti mwingi sana na muhimu umefanyika ndani tofauti na awali ulifanyika katika nchi zilizoendelea, hivyo ulikuwa hautusaidii kwa kiasi kukubwa kama huu unaotuhusu kabisa," alieleza.

Alisema uelewa wa wagonjwa wa selimundu umeongezeka ikiwamo kuanzishwa vyama vya wagonjwa, wazazi na vimeunganishwa kwenye mwavuli mmoja.

Vilevile, alisema sasa kuna programu inayohusisha mikoa saba kuchachua upimaji wa watoto wachanga wanaozaliwa kujua kama wana selimundu mapema.

"Lengo ni hadi ndani ya miezi sita wawe wamebainika ili kuwapatia matibabu mapema na kupunguza madhara ya ugonjwa huu," alisisitiza.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya, selimundu inachangia asilimia 6.7 ya vifo vyote vya watoto walio chini ya miaka mitano ikiwa ni sawa na watoto saba kati ya 100 wanaofariki dunia kila mwaka nchini.

## Tanzania yang'ara usimamizi rasilimali

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TANZANIA imetajwa kuwa na usimamizi mzuri wa rasilimali za madini hali inayovutia nchi mbalimbali kuja kujifunza namna zitakavyosimamia ili kunufaisha wananchi wao.

Waziri wa Madini na Maendeleo ya Migodi wa Zambia, Paul Kabuswe, alibainisha hayo jana alipokutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko.

Kiongozi huyo ambaye yupo nchini kwa siku mbili na ujumbe wake kujifunza usimamizi wa sekta hiyo na wachimbaji wadogo wa madini, alisema ziara hiyo inalenga kupeana uzoefu wa usimamizi wa madini yao ili yanufaishe wananchi wao.

"Sisi ni serikali mpya tupo kwenye ofisi kwa takribani miezi 10 kwa hiyo tumeona tuje kujifunza kwa kuwa miongoni mwa vitu ambavyo Tanzania imefanya vyema ni usimamizi wa rasilimali za madini wachimbaji wadogo," alisema.

Alisema wamekuja kujifunza namna watakavyosimamia sekta ya madini ya Zambia ili kuwanufaisha wananchi wake.

"Tumekuja kujifunza namna Tanzania inavyofanya kwenye leseni za madini na jinsi Stamico inavyofanya kazi na kuongoza sekta ya madini kwa kuwa Zambia kuna changamoto ya uchimbaji usiofuata sheria, tumekuja kujifunza ili tuondokane na changamoto hii," alisema.

Kwa upande wake, Waziri Biteko alisema, kiongozi huyo na ujumbe wake wapo nchini kujifunza usimamizi wa sekta ya madini hasa uchimbaji wa dhahabu na uchimbaji mdogo.

"Wenzetu Zambia wanatamani kubadilisha sera na sheria zao, ili madini waliyo nayo yawanufaishe, Zambia ni tajiri mkubwa wa madini ya dhahabu, shaba, koboti na mengine mengi, tutakuwa na waziri kwa muda wa siku mbili," alisema.

Alisema kuwa waziri huyo atakwenda kwenye machimbo kuangalia wanavyochimba wachimbaji wadogo na kutembelea masoko ya madini.

"Tunapokutana kwenye mikutano na tafiti nyingi zimefanywa Tanzania tumepiga hatua kubwa kwenye usimamizi wa sekta ya madini na misimamo ya viongozi wetu ambayo wameiweka juu ya usimamizi wa rasilimali umefanya usimamizi wa madini uwe mkubwa."

"Niliendа mkutano mmoja Capetown wawekezaji wakubwa walikuwa wakiitaja Tanzania kama mfano mzuri kwenye usimamizi wa sekta ya madini jambo ambalo tunajivunia na tutaendelea kuboresha zaidi," alisema.

# Mbunge Abood atoa misaada ya mamilioni

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MBUNGE wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood (CCM) ametoa msaada wa magari ya kubebea wagonjwa mawili yenye thamani ya Sh. milioni 172 ili kutoa huduma katika vituo vya afya Tungi na Lukobe katika Manispaa ya Morogoro.

Abood, akikabidhi vifaa vya maabara vyenye thamani ya Sh. milioni 9.7 kwenye Zahanati ya Tungi inayotoa huduma kwa mamia ya wananchi wa Kata ya Tungi, alisema atakabidhi magari hayo. Mbunge huyo aliongozana na Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Morogoro Mjini, ili kukagua ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kisasa cha Tungi kinachojengwa kupitia fedha zinazotokana na makusanyo ya ndani ya Manispaa ya Morogoro.

Alisema licha ya kwamba ujenzi wake bado unaendelea pamoja na kituo kingine cha Kata ya Lukobe, ameamua kuvipatia magari mapya ya kisasa ya kubebea wagonjwa ambayo yataanza kutoa huduma baada ya kukamilika kwa ujenzi wa vituo hivyo.

"Hiki kituo cha afya ni muhimu sana kwani kitasaidia kutoa huduma kwa wananchi na nipo hapa kwa ajili ya kutekeleza Ilani ya CCM, na leo (juzi) ninatoa vifaa vya maabara ambayo vimegharimu Sh. milioni 9.7," alisema.

Mbunge Abood alisema anafanya hivyo kwa kuwa haoni sababu za kuwa bahiri ilhali wananchi wa Mji wa Morogoro wanahitaji kutatuliwa kero zao.

Alisema Kata ya Tungi ina wananchi wengi na kwamba kujengwa kituo cha afya hicho mbali na kuwasaidia wakazi wa eneo hilo, pia kitakuwa msaada kwa wagonjwa wa kata zingine jirani.

"Tunahitaji hiki kituo kikamilike haraka ili kitoe huduma na iwapo manispaa ikikwama kupata fedha za kumalizia, nipewe taarifa ili niende wizarani nikaombe fedha ili kumalizia majengo ya kamilike... hatuwezi tukaishia kwa Sh. milioni 800 halafu tukashindwa kumaliza kituo cha afya," alisema Abood.

Mbunge huyo alitaka Kituo cha Afya Tungi kianze kutoa huduma za tiba kwa wananchi wa kata hiyo na zingine za jirani ifikapo Desemba mwaka huu.

Alisema kituo hicho cha afya kitakapoanza kufanya kazi, kutakuwa na wagonjwa ambao baadhi watatakiwa kupata rufani kwenda Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro.

Mbunge Abood alisema kuwa kwa kutambua hilo, magari hayo ya kisasa ya wagonjwa ambayo kila moja lina thamani Sh. milioni 86, yatatolewa kwa Kata za Tungi na Lukobe mara tu vituo hivyo vya afya vitakapokamilika.

Alisema Kituo cha Afya Lukobe awali kilipewa Sh. milioni 250 kwa ajili ya ujenzi, lakini fedha hizo hazikutosha kukamilisha ujenzi, hivyo alikiombea fedha nyingine Ofisi ya Rais - TAMISEMI na kufanikiwa kupatiwa Sh. milioni 250 zingine za kumalizia kituo hicho.

Diwani wa Tungi, Namala Mchunguzi, alisema kituo cha afya kinachojengwa katika kata yao ni cha mfano na cha aina yake mkoani Morogoro.



.Mbunge wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood (wa sita kulia), akabidhi vifaa vya maabara vyenye thamani ya Sh. milioni 9.7 kwa Mganga Mkuu wa Hospitali ya Manispaa ya Morogoro, Charles Rashid (kushoto kwake), kwa ajili ya matumizi ya zahanati ya Kata ya Tungi. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# GGML yajizatiti mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI nchini

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited (GGM) kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) inatarajia kukusanya Dola za Marekani milioni moja (Sh. bilioni 2.3) kupitia Kampeni ya GGM Kili Challenge 2022 inayotarajiwa kuanza Julai 15 hadi 21 mwaka huu.

Vilevile, GGML imeahidi kuendelea kushirikiana na serikali kupitia TACAIDS pamoja na wadau wengine kuendeleza mapambano dhidi ya Virusi Vya UKIMWI (VVU) na UKIMWI ili kufikia malengo ya sifuri tatu.

Malengo ya sifuri tatu yanamaanisha kupunguza kabisa kwa kufikia asilimia sifuri ya maambukizi mapya, sifuri ya unyanyapaa pamoja na sifuri katika vifo vitokanavyo na UKIMWI.

Kauli hiyo ilitolewa juzi jijini Dodoma na Meneja Mwandamizi wa Masuala ya Ubia kutoka GGML, Manace Ndoroma, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uzinduzi wa kampeni ya GGM Kili Challenge kwa mwaka 2022. Kampeni hiyo iliyoasisiwa na GGML mwaka 2002, inalenga kutunisha Mfuko wa Mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI kwa kukusanya fedha ili kuisaidia Serikali ya Tanzania katika jitihada zake kufikia malengo ya sifuri tatu.

Kampeni hiyo pia inalenga kuendeleza mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI nchini na kushirikisha wadau kuchangia mwitikio wa Taifa dhidi ya VVU na UKIMWI.

"Washiriki watapanda Mlima Kilimanjaro kuanzia Geti la Machame kwa njia ya miguu na wengine kwa baiskeli kisha kushukia Geti la Mweka mkoani Kilimanjaro. Tunawakaribisha sana wadau wetu na kampuni mbalimbali kuchangia na kushiriki kampeni hii," alisema.

Aliishukuru Serikali ya Tanzania kwa msaada wake na ushirikiano wa TACAIDS katika kampeni ya Kili Challenge tangu kuanzishwa kwake mwaka 2002.

"Takwimu za kitaifa za watu wanaoishi na VVU hujumuisha hata wale wanaoishi mkoani Geita, ndiyo maana tunafanya jitihada za pamoja kutokomeza maambukizo mapya nchi nzima," alifafanya Ndoroma.

GGM Kili Challenge imepiga hatua tangu kuanzishwa kwake mwaka 2002 hadi kufikia kuwa mfuko wa kimataifa, wenye kushirikisha wapanda mlima na waendesha baiskeli zaidi ya 700 kutoka mabara sita na zaidi ya nchi 20.

Alisema kampeni hiyo ya GGM Kili Challenge ni mojawapo ya majukumu yanayotekelezwa na kampuni hiyo katika kuchangia miradi mbalimbali ya kijamii ambapo kila mwaka hutumia Sh. bilioni tisa hadi 11.

Mkurugenzi Mkuu wa TACAIDS, Dk. Leonard Maboko, katika kuhamasisha wananchi kulipa kodi na kutunisha Mfuko wa Mapambano dhidi ya VVU, alisema serikali imefanya marekebisho ya sheria ya kodi ambapo sasa wadaiwa au kampuni zinazodaiwa kodi na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) zinaweza kupata msamaha wa kodi kwa kuchangia mfuko huo.

"Kwa mfano, kama kampuni inadaiwa kodi Sh. milioni 100, ikitoa Sh. milioni 50 kuchangia Mfuko wa UKIMWI, itahesabu amelipa kodi, hivyo kule TRA deni lake litabaki Sh. milioni 50 pekee," alisema.

Aliongeza kuwa serikali imechukua hatua hiyo kwa kuwa licha ya mafanikio yaliyofikiwa katika mapambano ya UKIMWI, bado ni tatizo nchini, hivyo fedha zinahitajika kutokomeza janga hilo.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwapo kwa ongezeko la maambukizi mapya ya VVU hususan kwa makundi maalum yaliyo katika hatari kubwa ya maambukizi.

Mkurugenzi Mkuu huyo alibainisha kuwa hadi kufikia mwaka 2020, idadi ya Watanzania wanaoishi na VVU nchini ilifikia 1,700,000 na maambukizo mapya kwa mwaka ni watu 68,000.

Alisema kupitia kampeni ya GGM Kilimanjaro Challenge, taasisi mbalimbali zimenufaika kwa kupata fedha za kutekeleza shughuli za mwitikio wa VVU na UKIMWI nchini.

Kwa mfano, mwaka 2020 Mfuko wa Kilimanjaro Challenge ulitoa fedha taslimu Sh. milioni 800 kwa taasisi 20 zisizo za kiserikali.

Asasi hizo zimetekeleza miradi mbalimbali iliyowalenga vijana, watu wanaoishi na VVU, watoto yatima na waliopo kwenye mazingira magumu pamoja na jamii kwa ujumla. Zaidi ya watu 1,000 wamenufaika kutokana na fedha hizo.

## Bashe aagiza ufuatiliaji mashamba ya ngano

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amewaagiza wakuu wa mikoa kufuatilia mashamba yote na idadi ya wakulima wa ngano ili kufikia lengo la serikali la kulima hekta 400,000 za zao hilo kwa kipindi cha miaka mitatu.

Wizara hiyo pia imetoa tani 50,000 za mbegu ya ngano ili kuchochea uzalishaji wa zao hilo nchini.

Bashe, alibainisha hayo jana wakati akizungumza na wadau wa zao hilo kutoka mikoa mbalimbali nchini pamoja na wakuu wa mikoa inayolima na kustawi zao hilo. Alisema kufanya hivyo ni moja ya mikakati ya serikali ili kuhakikisha inachochea na kuongeza idadi ya wakulima pamoja na uzalishaji wa ngano nchini.

"Hekta 400,000 kwa ajili ya kilimo cha ngano zilikuwapo isipokuwa wakulima walikuwa hawafuatilii ndiyo maana serikali imeamua kuingilia kati ili kuhakikisha zinatambulika na wakulima wazitumie ipasavyo," alisema Bashe.

Hata hivyo, Bashe alisisitiza kuwa wilaya na mikoa ambayo ngano inastawi, waweke mkazo kulima zao hilo kutokana na soko kubwa ndani na nje ya nchi.

Hata hivyo, aliwataka wakuu wa mikoa wakawatambue wakulima na kuona ngano inakusanywa kwenye ubora wa aina ipi ili kulinda suala la ubora kwenye zao husika.

"Kuonyesha msisitizo wa zao hilo ngano Limited tumeshirikiana na kukubaliana naye na tayari amefungua ekari 27,000 msimu huu," alisema Bashe.

Alisema mwaka jana walikuwa na mkutano na wadau na walianza majaribio Mkoa wa Manyara, wanaona unakuja na matokeo mazuri.

"Tunatengeneza mazingira ili mzalishaji anunue ngano ya ndani na ili mkulima aweze kuzalisha anatakiwa kuwa na soko la uhakika, mbegu na uhakika wa bei," alisema Bashe.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omar Mgumba, alisema kuwa maeneo ya Igamba na Magamba katika mkoa huo yalikuwa yakizalisha ngano kwa wingi.

Mgumba, alisema kuwa pamoja na maeneo hayo kulima ngano, lakini waliacha baada ya kuona ni mazao gani yanawapatia faida kiuchumi na kuanza kulima mengine ikiwamo mahindi.

"Ardhi iko kubwa kwangu Songwe, lakini inatafutwa kwa tochi matokeo yake wanavamia misitu ya hifadhi na ili tuwe na uhakika Wizara ya Ardhi ifanye tathmini ni ardhi ipi inafaa kwa kilimo hicho," alisema.

# Wamlalamikia RC kutozwa gharama tofauti kujifungua jinsi ya kike, kiume

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

WANANCHI wa Kijiji cha Misigiri, Kata ya Ulemo wilayani Iramba, mkoani Singida wamelalamika wajawazito wanapokwenda kujifungua katika Hospitali ya Wilaya ya Kiomboi, kutozwa Sh. 60,000 anapozaliwa mtoto wa kiume na Sh. 50,000 kwa mtoto wa kike.

Pia anapojifungua kwa operesheni anatozwa kati ya Sh. 200,000 hadi 300,000 hali ambayo inasababisha wengine kushindwa kumudu gharama kutokana na hali ya maisha.

Walitoa malalamiko hayo kwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Bilinith Mahenge, wakati akizungumza na wananchi hao kwenye mkutano wa hadhara katika mfululizo wa ziara ya kusikiliza kero.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa tunatozwa fedha nyingi tunapowenda kujifungua katika Hospitali ya Wilaya ya Kiomboi, mfano anapozaliwa mtoto wa kiume tunatozwa Sh. 60,000 na mtoto wa kike Sh. 50,000, operesheni 200,000 hadi 300,000 tunaomba utusaidie kwa hilo," alilalamika, Maria Isaya.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Singida, Hyasinta Alute, akijibu suala hilo alimwahidi Mkuu wa Mkoa kuwa watalifuatilia kujua mama huyo alitozwa fedha hizo katika kituo gani. Kutokana na hali hiyo, Dk. Mahenge, alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda, kufuatilia suala hilo waangalie huduma za mama kujifungua zinavyotolewa na kama wanatoa stakabadhi.

"DC fuatilia suala hili mjue kama wapo watu wanakiuka taratibu basi hatua zichukuliwe haraka," alisema Dk. Mahenge.

Alisema inasikitisha gharama za kujifungua mtoto wa kiume na wa kike na upasuaji na kuahidi kuwa serikali itafuatilia suala hilo na kuchukua hatua kwa wahusika.




Ofisa Miradi wa Asasi ya Vodacom Tanzania Foundation, Salome Mtali (kulia), akitoa maelezo kwa watendaji na wakuu wa idara mbalimbali za kampuni ya Vodacom Tanzania Plc, kuhusu namna huduma ya m-mama inavyofanya kazi, walipotembelea banda la kampuni hiyo kwenye maonyesho ya 46 ya kimataifa ya biashara Dar es Salaam jana. Huduma hiyo inawagusa kinamama kwa kuwapa usafiri pindi wapatapo dharura wakati wa ujauzito ama kujifungua. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyabiashara EAC waomba kuondolewa vikwazo kibiashara

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

BAADHI ya wafanyabiashara wanaoshiriki Maonyesho ya Biashara ya nchi za Afrika Mashariki (EAC's EXPO Bukoba) wameiomba serikali nchini kuwaondolea vikwazo vya kibiashara ikiwamo wingi wa vizuizi barabarani na kulipia mzigo mmoja mara mbili.

Wakizungumza katika viwanja vya CCM yanakofanyika maonyesho hayo, wafanyabiashara hao walisema kuwa vikwanzo vingi wanakutana navyo mipakani, na kutoa mfano waliwahi kukaa siku tatu katika mpaka wa Rwanda na Tanzania wakati wakienda nchini humo, hadi mabalozi wa mataifa hayo walipofika na kuzungumza na maofisa wa Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) na kuruhusiwa.

"Mwaka huu tunaenda Uganda, tutaangalia mpakani wakati wa kwenda na kurudi kama vikwazo vitapungua, maana wakati mwingine tunalipia mzigo ule ule mara mbili, wakati unaenda nao ukibakia wakati unarudi unaambiwa ulipie tena mpakani," alisema mmoja wa wafanyabiashara hao, Judith Rugamba.

Mfanyabiashara Minani Frolibert kutoka Bujumbura nchini Burundi aliomba Serikali ya Tanzania kuweka mazingira ya kuwawezesha taasisi yake kuja kuwafundisha vijana ujasiriamali ili waweze kujiajiri.

"Sisi ni wana sanaa na kwetu Burundi tuna vijana 50 ambao tunawafundisha namna gani watajikwamua katika umaskini kupitia sanaa, tungepata ushirikiano tungetoa mafunzo kwa vijana wa Tanzania kwa sababu kwa sasa wanapenda kujiajiri," alisema Frolibert.

Mratibu wa maonyesho hayo, William Rutta, aliwashukuru wafanyabiashara kutoka nchi za Afrika Mashariki kwa mwitikio wao mkubwa, na wanatarajia idadi ya wafanyabiashara kuongezeka.

"Pamoja na wafanyabiashara kukutana, kutangaza bidhaa zao, lakini wanabadilishana uzoefu na kupewa elimu ya namna gani wanaweza kupiga hatua mbele zaidi kupitia shughuli za ujasiriamali," alisema Rutta.

Akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Kagera wakati wa ufunguzi rasmi wa maonyesho hayo, Mkuu wa Wilaya ya Muleba, Toba Nguvila, alizitaka mamlaka husika ikiwamo TRA kupunguza vikwazo kwa wafanyabiashara ikiwamo vizuizi vya barabarani.

"Unakuta mfanyabiashara anataka kwenda Uganda, hapa Bukoba amezuiwa, Missenyi amezuiwa, Custom amezuiwa, na wakati mwingine anatumia siku mbili au tatu, akitoka pale anakwenda Mbarara anazuiwa kabla hajafika hata Kampala, hivi vikwazo vya kibiashara ambavyo vinaleta ugumu kwa wafanyabiashara wetu katika kufikia soko la Afrika Mashariki ni vizuri viondolewe," alisema Nguvila.

Maonyesho hayo ya Afrika Mashariki yalianza Juni 22 katika Manispaa ya Bukoba na yanatarajiwa kufikia kilele Julai 08, mwaka huu, ambapo yamewashirikisha wafanyabiashara kutoka nchi za Uganda, Rwanda, Burundi, Kenya, Jamhuri ya Kidemokrasia Congo na mwenyeji Tanzania.

# Wabunge waibana serikali kuhusu tembo waharibifu

WABUNGE wameibana serikali kueleza mkakati wa kudhibiti tembo waharibifu mali na kuua watu kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Wakiuliza maswali bungeni jana, Mbunge wa Kilwa Kaskazini (CCM), Francis Ndulane, alihoji serikali ina mpango gani wa kudhibiti tembo wanaoharibu makazi na mashamba katika Kata za Kandawale na Miguruwe ambazo zinapatikana katika Pori la Akiba Selous.

Naye Mbunge wa Mlalo (CCM), Rashid Shangazi, alisema katika kata za Lunguza, Mlalo na Mlazi ambazo zipo jirani na hifadhi ya Mkomazi, tembo wanavamia na jana walikuwapo na kuomba kupatiwa kituo cha askari wanyamapori.

Kwa upande wake, Mbunge wa Meatu (CCM), Leah Komanya, alihoji serikali haioni haja ya kufika Meatu kuona uharibifu mkubwa unaofanywa na tembo kwenye mashamba ya wananchi yenye mizinga ya nyuki na watu wawili wameuawa na tembo hivi karibuni.

Pia Mbunge wa Tunduru Kusini (CCM), Daimu Mpakatye, alisema tembo wameweka kambi ya muda mrefu katika kata mbalimbali za jimbo hilo na kuhoji lini serikali itajenga kituo cha askari kudhibiti wanyama hao ili kuondokana na maafa ya tembo kila mwaka.

Vilevile, Mbunge wa Viti Maalum, Grace Tendega, alihoji mpango wa serikali wa kudhibiti wanyama hao na kulipa fidia wananchi, hivi karibuni wananchi wawili wa Jimbo la Isimani wameuawa.

Mbunge wa Viti Maalum, Cecilia Paresso, alisema tatizo la tembo kuvamia na kuua watu ipo pia Wilaya ya Karatu na kuhoji mkakati wa serikali kudhibiti tembo hao.

Akichangia hoja hiyo, Mbunge wa Bunda (CCM), Boniphace Getere, alisema jimbo hilo linaongoza kwa kuathiriwa na tembo nchini na kutaka vituo vya askari wa kudhibiti wanyama hao kuzunguka eneo hilo.

Mbunge wa Viti Maalum, Tunza Malapo alisema kutokana na ongezeko la tembo hao kwa sasa kufanya uharibifu lini serikali itaanza utaratibu wa kuwavuna.

Akijibu maswali ya wabunge hao, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, alisema katika kukabiliana na tatizo hilo, wizara imeanza kujenga vituo vya askari wanyamapori katika maeneo mengi nchini kwa lengo la kuwa karibu na wananchi ili kuwadhibiti wanyama hao.

Alisema kwa mwaka 2020/21 tayari vituo 19 vimejengwa na kwa mwaka 2022/23 vinatarajiwa kuongezwa vituo 13.

Alisema wizara imepata kibali cha kuajiri askari 600 ambao watasambazwa kwenye maeneo hatarishi.

Pia wizara itaendelea na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu mbinu za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu. Hata hivyo, alisema kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu hasa jirani na maeneo ya hifadhi kumechochea wanyama hao kuwa waharibifu.

Kadhalika, alisema idadi ya wanyama hao kwasasa inakaridiwa kuwa 55,000 na haijafikia iliyokuwapo mwaka 2009 ya 134,000.

"Kwa kuwa kumekuwa na ongezeko la wananchi ambao wanasogea maeneo ya hifadhi sambamba na shughuli za binadamu, na usumbufu wa tembo ni kati ya mwezi Aprili na Julai ambapo ni kipindi cha mavuno na wataalamu wanasema wanyama hawa hunusa kwa takribani kilometa 200, tunaamini mazao yanapoiva tembo wanahamasika kwenda na si kweli kwamba wameongezeka," alisema.

Masanja alitaka wananchi wanaodai kifuta machozi na jasho kutoa taarifa ili kulipwa kwa wakati.



Mbunge wa Geita Mjini, Constantine Kanyasu, akiuliza swali kwenye kipindi cha maswali na majibu wakati mkutano wa saba kikao cha 55 cha Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Samaki wapungua Bwawa la Nyumba ya Mungu

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imekiri kupungua kwa samaki katika Bwawa la Nyumba ya Mungu huku ikitaja mikakati mitatu iliyochukuliwa kuondokana na hali hiyo.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Abdallah Ulega, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Moshi Vijijini (CCM), Prof. Patrick Ndakidemi.

Mbunge huyo alihoji mkakati wa serikali wa kukabiliana na kupungua kwa idadi ya samaki katika bwawa hilo ili kusaidia wananchi wanaotegemea uvuvi.

Akijibu swali hilo, Ulega alisema kutokana na wingi wa watu na mahitaji, idadi ya samaki imepungua na hatua zinazochukuliwa ni kudhibiti uvuvi haramu.

"Tumeelekeza taasisi ya utafiti wa uvuvi kuangalia uwezekano wa kupandikiza zaidi samaki na kupeleka programu ya vizimba ili wananchi wale wanufaike na rasilimali hizi za samaki," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Kigamboni (CCM), Dk. Faustine Ndugulile, alihoji serikali ina mpango gani wa kujenga soko kubwa la samaki katika Wilaya ya Kigamboni.

Akijibu swali hilo, alisema kwa mwaka wa fedha 2022/23, serikali imetenga fedha za kujenga soko hilo.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Neema Mgaya, alihoji lini serikali itajenga miundombinu rafiki ya kufanya biashara ya samaki pamoja na kuhifadhia vifaa vya uvuvi (mwalo) katika kata ya Ruhuhu iliyoko wilayani Ludewa.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Ulega alisema katika mwaka 2022/23 wizara hiyo itatuma wataalamu wake wilayani Ludewa ili kufanya upembuzi yakinifu wa athari za mazingira na jamii wa maeneo yanayofaa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu rafiki ya uvuvi ikiwamo mialo, masoko, maghala na sehemu za kuhifadhi vifaa vya uvuvi.

"Lengo ni kuwawezesha wavuvi na wafanyabiashara wa samaki na mazao ya uvuvi wa Wilaya ya Ludewa ikiwamo Kata ya Ruhuhu kufanya shughuli zao kwa ufanisi na tija," alisema.

Hata hivyo, alisema baada ya kukamilika, wizara itashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kuanza ujenzi wa mwalo mmoja katika eneo litakalooneka-na linafaa wilayani humo na ambalo wananchi wataridhia kutoa ardhi bila fidia.




**Habari zote: Augusta Njoji DODOMA**

## TAMISEMI yafafanua wanafunzi waliopangiwa vyuo

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema hakuna mwanafunzi aliyepangiwa kwenda chuo cha kati bila yeye kuomba.

Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, David Silinde aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Geita Mjini (CCM), Constantine Kanyasu.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema hivi karibuni serikali ilipanga vijana waliomaliza kidato cha tano na wengine kwenda vyuo, lakini wanafunzi hao wenye ufaulu wa daraja la kwanza na pili kwenye masomo ya sayansi wamepelekwa vyuo vya kati bila wao kupenda na wakiomba kubadilisha kwenda kidato cha tano utaratibu ni mrefu.

"Ni kwanini serikali isibadilishe utaratibu kwamba wanaotaka kwenda vyuo vya kati wachague wenyewe," alihoji.

Akijibu swali hilo, Silinde alisema wanafunzi wenyewe ndiyo waliojaza chaguo la kwanza kwenda vyuo vya ufundi na baada ya kufaulu mtihani wa kidato cha nne walitaka kubadili kwenda kidato cha tano badala ya machaguo yao ya awali.

"Serikali haikuwapeleka wanafunzi waliopata daraja la kwanza na la pili kwa makusudi bali mifumo ipo ambayo waliomba na walipewa fursa ya kuingia kubadili baada ya matokeo," alisema.


Awali, katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Zuena Bushiri, alihoji lini serikali itaongeza watumishi wa Kada ya Uhandisi na Fundi Sanifu kwa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), Mkoa wa Kilimanjaro.

Akijibu swali hilo, Silinde alisema TARURA Mkoa wa Kilimanjaro ina wahandisi 18 na upungufu wa wahandisi nne na mafundi sanifu sita.

Aidha, alisema serikali imepeleka wahandisi watatu katika Mkoa wa Kilimanjaro walioajiriwa kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Alisema TARURA itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kuwezesha upatikanaji wa vibali vya ajira za watumishi wa kudumu na hivyo kuweza kutatua tatizo la upungufu wa watumishi katika Mkoa wa Kilimanjaro na mikoa mingine.

Ukurasa 13




Hatuko kwenye kodi pombe, kinachotozwa sasa ni kamari!



## Mahali ilikosimama zama za kukabili makali uchumi na bunge lenye mageuzi ya uchumi

Ukurasa 12

BUFE
IJUMAA JULAI 1, 2022
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

JENGA AMANI

# Mradi unaohamisha watu kutoka migogoro hadi penye maendeleo

**Na Julieth Mkireri**

UNAUJUA mradi wa Jenga Amani uliofungwa hivi karibuni? Ni uliokusudia kujenga ushirikiano wa asasi za kiraia, vyombo vya habari, viongozi wa dini na serikali katika kuelezea vitu na matatizo yahusuyo migogoro, hata kukuza maendeleo kwa umma.

Ni Mradi ulioanza kutekelezwa mwaka 2020 ukiwafikia walengwa katika wilaya za Rufiji na Kibiti mkoani Pwani; Tandahimba na Mtwara Mjini, mkoani Mtwara; Tarime, Mara; pia Zanzibar (Unguja na Pemba).

Mradi uliainisha migogoro, ikiwemo vyanzo vyake na maeneo husika. Mbinu zake, ulilenga kuelimisha kila kundi nafasi za ushirikishwaji katika kutatua matatizo kwenye maeneo ya mradi.

Makundi yaliyolengwa katika mradi huo yametokana na nafasi yake ya ushawishi kwenye jamii na mfadhili wa mradi huo ni Umoja wa Ulaya (EU) ukitekelezwa na Shirika la Search For Common Ground Tanzania.

Hapo ilishirikiana na Kituo cha Msaada wa Kisheria Zanzibar na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kwa takriban miezi 30, wadau mbalimbali walilengwa na kujengewa uwezo.

Wakati ndio umefungwa wiki hii, unatajwa kubadilisha mtazamo namna watu mbalimbali kuhusiana na utatuzi wa migogoro, huku wanufaika katika mkoa wa Pwani wakikiri kuwa wameona umuhimu kuepuka migogogoro na machafuko na kuitatua kwa njia ya ushirikishwaji, sasa wanajikita katika maendeleo na uchumi .



Kada ya vijana wakiwa mitaani. Ni sehemu ya wanaolengwa na mradi tajwa, kuhamia kwenye uchumi na maendeleo. **PICHA: MTANDAO**

Erasto Joseph, mkazi wa Rufiji, anaeleza kabla ya mradi kulikuwapo matatizo ya uvunjifu wa amani na kutokana na jamii kutokuwa na elimu ya namna ya kutatua migogoro, iliendelea na kuleta machafuko.

Erasto anaeleza kwamba, baada ya mafunzo mbalimbali waliyopata, sasa wananufaika kutatua migogoro kwa njia ya amani, baada ya kufundishwa masuala ya kuwa kila mtu ana haki mbele ya mwingine.

Anasema, elimu iliyotolewa katika mradi wa Jenga Amani, pia ameifikisha kwenye makanisa na kuwafikia vikundi anavyofanya navyo kazi, huku elimu imeendelea kusambaa kwa kila mmoja akisisitiza amani, na kutatua migogoro kwa ushirikishaji, ikimalizika kwa maelewano na watu kuangukia njia ya maendeleo.

Mwingine, Rajab Mlawa wa Mkuranga, anasema kanufaika kupitia elimu hiyo na sasa wameanza kuitumia kutatua migogoro ngazi ya familia.

Rajab anayetoka katika asasi ya Kiraia ya Kikale Youth Centre, anasema katika asasi yao inayojishughulisha na vijana walioathirika na dawa za kulevya, walibaini baadhi yao wamejiingiza huko kutokana na migogoro ya kifamilia, hata wakaweka kando shughuli za uchumi .

Anasema baada ya mafunzo hayo amekuwa akiyatumia kusuluhisha migogoro anafafanua: "Tumeanza kuitumia migogoro kama fursa na si tatizo tunaishughulikia kuanzia ngazi ya familia na tumeanza kupata matokeo chanya."

Naye, Mariasha Juma anasema elimu imewasaidia kuwakusanya watu wenye migogoro na kutatua vikwazo vinavyowakabili na kupata matokeo chanya.

"Nashukuru elimu niliyopata kutoka mradi wa Jenga Amani yetu imesaidia kukutana na wahusika kwenye mgogoro kuongea na kila pande na baadae kuwakutanisha kwa pamoja"anaeleza.

Kwa mujibu wa Mariasha, sasa anaitumia elimu akiwa kwenye nafasi yake ya mjumbe wa Baraza la Usuluhishi la Kata, ambako kuna migogoro mingi ya ndoa.

"Kwenye migogoro ya ndoa natumia elimu yangu na wenzangu kuongea na wahusika kila mmoja kwa nafasi yake athari ambazo zinaweza kutokea kwa watoto endapo wataachana na baadae kuwakutanisha pamoja na kusuluhisha hii ni moja ya matokeo chanya kwangu" anaeleza Mariasha.

Gustaf Haule ni kati ya Waandishi wa Habari wa Mkoa wa Pwani wanufaika wa elimu ya kupitia Mradi wa Jenga Amani, yetu ambaye anasema kwa sasa kabla ya kuandika habari za migogoro pia kwa nafasi yake atatumika kuitatua kwa kuanza kusikiliza kila upande na baadae kuwakutanisha wahusika.

"Mradi umesaidia kutupa mwanga kuhakikisha tunapunguza vikwazo vya migogoro kwa wananchi na kuleta amani,hususani sisi wanahabari hatuna budi kuwa na jicho la tatu katika jamii"anaeleza.

Johson Mbwambo, ni Ofisa Miradi Msaidizi wa shirika la kimataifa la Search for Common Ground anayehudumu katika Mkoa wa Mtwara ambaye anaamini kuwa washiriki wa mradi na jamii ya ndani na nje ya Mtwara, watakuwa wamenufaika kupitia masuala mbalimbali.

Anawakumbusha wanufaika kuendelea kutumia elimu waliyoipata kuhamasisha amani ili kuepusha kuendelea kushamiri kwa migogoro na kusababisha kudumaza shughuli za maendeleo na kuondoa amani kwenye maeneo husika.

UCHUMI

# Mahali ilikosimama zama za kukabili makali uchumi na bunge lenye mageuzi ya uchumi

## • Mwelekeo mpya ni kilimo na 'mafuta' mapya

**Na Peter Orwa**

JANA ndio kikao cha Bunge la Bajeti kilifungwa rasmi jijini Dodoma, kwa hotuba ya kina ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambayo katika moja ya mambo aliyoyaweka bayana, ni uamuzi wa kiuchumi kuhamishwa jamii kutoka Pori Tengefu la Loliondo, hadi makazi mapya wilayani Handeni.

Wilaya hiyo ya mkoani Tanga, kimazingira inajulikana kuwa rafiki kwa kilimo cha mazao mengi, wakati huohuo panaendana na ufugaji. Hata kabla ya uamuzi huo wa serikali, mahali hapo kumepatikana baadhi ya wafugaji walio wakazi wa muda mrefu.

Ni aina ya hatua ya kihistoria inayogusa sura ya kimataifa katika eneo hilo, wakazi wake wote ambao kimsingi wamekuwa jamii ya wafugaji.

Wahamaji hao wamehama kwa hiari wakapewa nyumba zenye vyumba vitatu vya kulala katika makazi mapya, kila mmoja anapatiwa eneo ekari mbili na nusu ya kulishia mifugo, pamoja na kuwepo maeneo ya wazi ambayo wakazi waliohama kwa hiari wanakiri yamewafaa, huku wakipata makazi ya ziada kwa ajili ya mifugo.

Makazi hayo wakati ambapo mwaka 1959 yalikuwa sehemu ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, kukiwapo wakazi 8,000 wa mahali hapo na makazi jirani, lakini hadi kufika mwaka jana, tayari kulishaundwa chombo kingine, Mamlaka ya Pori Tengefu Loliondo, ikiwa na wastani wa wakazi 120,000.

Kimsingi, Mamlaka ya Pori Tengefu Loliondo, iko jirani na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, ambayo sasa wakazi wake wanahamia Handeni kwa utaratibu wa hiari, huku mjadala wake ukiwa mkubwa na serikali, ikitoa ufafanuzi wa kina kila mara, ikiwamo jana bungeni, kupitia Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (aliyeinama), akikagua kitalu cha uzalishaji wa miche ya michikichi katika kambi ya Jeshi Bulombora mkoani Kigoma

### KUKABILI MAKALI

Hayo yanatokea, huku Rais Samia Suluhu Hassan ameshatoa angalizo la uchumi wa kimataifa, namna Tanzania haiwezi kuwa kisiwa kutokana na vita vinavyoendelea vya mataifa ya Ukraine na Russia, lazima itaathirika kiuchumi.

Kabla ya hata kuanza vikao vya bunge vilivyoisha jana, kukashuhudiwa kuongezeka bei ya mafuta ya petroli na ngano ambayo kwa kiasi kikubwa inatoka ukanda huo.

Yote yakaibua mijadala mikubwa ya umma hadi nje ya nchi kuhusu hali ya kiuchumi gharama za baadhi ya vitu, ikiwamo petroli, huku vikao vya bunge vilipoanza, navyo vikashika hoja hiyo, hali inayoendana na ufafanuzi wa kiserikali.

Hatua mojawapo ya kutoa nafuu kwa magumu ambayo yanagusa moja kwa moja maisha ya umma, Rais Samia akaingilia kati suala la mafuta kuipa nafuu, serikali kuingiza Sh. Bilioni 100 ya ruzuku ili kupunguza makali ya kupanda bei ya huduma hiyo muhimu kitaifa.

Jambo hilo linachukua nafasi, huku kilio hicho ambacho kinagusa hadi ughaibuni kwa makali zaidi, mamlaka za kusimamia usafiri nchini ilichukua nafasi kuvipa nafuu vyombo vya usafiri, kwa kuongezwa nauli, mfano jijini Dar es Salaam, kuwa na ziada ya Sh. 100 ya bei ya awali.

Ni hali inayochukua sura, huku katika baadhi ya nchi jirani ya Afrika Mashariki magumu yakichukua sura mapema zaidi na hata kukabiliwa na hatua mbaya zaidi kwa bidhaa hiyo ya mafuta, kukosekana vituo vyake vyake vya huduma.

Nchini, siku chache zilizopita baada ya kuingizwa ruzuku hiyo ya mafuta, kumeshuka kiasi bei ya mafuta nchini, hali inayosaidia kupunguza makali ya gharama hizo, ikiwa nayo ni hatua inayoanzia katika uamuzi wa Rais Samia, kukabili makali hayo.

### MAFUTA YA KULA

Eneo lingine ambalo limeibua mageuzi katika maisha ya jamii kupitia kikao cha bajeti ya mwaka huu, mengi yamo katika uwasilisho wa Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, kuanzia leo ni rasmi kuandaliwa mazingira nafuu ya bei katika mafuta ya kula.

Kwa mujibu wa uwasilisho huo wa Waziri wa Fedha na Mipango hivi karibuni kumeondolewa kodi nyingi, ili kutoa nafuu ya bei kutakopanua soko la uzalishaji nchini na nafuu ya maisha kwa watumiaji.

Itakumbukwa, kutokana na uzalishaji mdogo wa mafuta ya kula hata nchi kutegemea zaidi bidhaa hiyo kutoka nje, serikali iliingiza mafuta katika mazao ya kimkakati uzalishaji mafuta, hasa kwa mazao kama ya mchikichi na alizeti.

Hadi sasa hatua hiyo serikali inafuatilia kwa namna ya kipekee, na Waziri Mkuu Majaliwa akiwa mfano katika hilo, akizuru maeneo mbalimbali nchini penye uzalishaji na kuelekeza la kufanyika.

Pia, asasi za umma kama vile vyombo vyake; Jeshi ka Kujenga Taifa (JKT) na jeshi la Magereza, zilizama zaidi katika kuibua mashamba ya mazao hayo.

Ni aina ya mashamba ya kuzalisha mafuta na mbegu bora, chini ya usaidizi wa kitaalamu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI), ushuhuda wake ukiwamo katika mashamba yanayopatikana wilayani Kilosa, Morogoro, pia Kigoma na Dodoma.

Vivyo hivyo, hatua za msamaha wa kodi na ujenzi wa mazingira rafiki katika kuikusanya kodi nchini, ambazo zimekuwa zikitangazwa katika matukio mbalimbali nchini, ikiwemo na mawaziri bungeni, mpaka mamlaka za juu zinatajwa kupanua wigo na mzunguko wa fedha.

Rais Samia hivi karibuni akiwa ziarani mikoani, alikumbusha mamlaka za kiserikali zinazohusika na utozaji kodi, kujenga mazingira rafiki katika wajibu huo, ikiwa ni namna ya kusisimua uchumi, biashara na uzalishaji.

Waziri mwenye dhamana katika hatua inayoendana na hiyo, akasema bungeni siku chache baadaye kwamba, serikali itachukua hatua ya kutambua walipa kodi wazuri na kuwasamehe inapobidi, katika kodi zilizopita.

### NEEMA YA KILIMO

Sekta ya Kilimo, nayo mwaka huu imeguswa na uhamasishaji huo, pia uzalishaji wake kuhamishwa kwa ukubwa kutoka serikalini, hata kufungua sura pana namna ambavyo kilimo kinatarajiwa kupanuka, ikirejewa dhamira za awali, ambazo zimeshachukua nafasi, mfano hai katika malengo yanayoendela kuwekwa katika mafuta ya kupika.

Kilimo kinachopatikana kijijini, ni eneo ambalo serikali inaendeleza hatua kubwa ikipigania vita vya umeme vijijini kupitia mradi wake uitwao REA, hali inayotarajiwa kuinua maeneo hayo, ambako ndiko kwenye mzizi wa kilimo.

Mengine ambayo yanaonekana ya mkazo katika awamu ya uongozi wa serikali hivi sasa, ni maboresho ya bandari mbalimbali nchini, ikiwamo ya Kalema, iliyoko Katavi, ikiaminika italeta mabadiliko makubwa ya kimaendeleo.

Ni hatua zinazoendana na simulizi nyingine nyingi za maboresho kama hayo katika Bandari kubwa za Tanga na Mtwara, zikiibadilisha nchi katika sura mpya zaidi ya hatua ya kiuchumi.




Mradi wa Umeme Vijijini (REA), ukiendelea ukiwa ni kichocheo cha kuwania maendeleo. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



TAFAKURI YA MLALAHOI

# Hatuko kwenye kodi pombe, kinachotozwa sasa ni kamari!






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
jkulangwa@yahoo.com

MIAKA kadhaa iliyopita, kila hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali ilikuwa kawaida kila waziri mwenye dhamana ya fedha, kutamka ongezeko la bei ya vinywaji, hususan pombe na sigara.

Watu walikuwa wakijiandaa kusikia bei mpya ya bia na mvinyo na baadhi wakinywa sana siku moja kabla ya siku ya bajeti, kwa imani kwamba kuanzia siku hiyo bei itapanda.

Ingawa haikuwa hivyo kwamba bei inapanda sawia, ila mpaka kuanza kwa mwaka mpya ambao ni Julai Mosi, lakini wanywaji walifanya hivyo kuonyesha kuwa ni lazima bei mpya itangazwe.

Ilikuwa kawaida ikionyesha kuwa serikali ilitegemea zaidi vinywaji kama vyanzo muhimu vya mapato na ndiyo sababu bei ilipanda kila mwaka wa fedha. Hivyo, viwanda vya vinywaji na sigara vikaonekana ni tegemeo kwa uchumi wa nchi.

Alipoingia madarakani Rais Dk John Magufuli mwaka 2015 akachukua hatua zinazohusiana na unywaji, pale alipozuia mchezo wa 'pool table' ambao zaidi upo baa, wachezaji zaidi vijana uendeshwe kwa muda maalum ulioruhusiwa .

Ikatangazwa kuwa ufunguaji baa uzingatie muda wa kazi na hata uchezaji 'pool table', mvinyo vivo hivyo. Wenye baa wakaambiwa mtu asionekane anakunywa bia au pombe yoyote, kabla ya muda wa kufungua baa saa 10.00 jioni.

Wakaambiwa, asionekane mtu akicheza 'pool table' kabla ya muda huo, kwani Rais alibaini kuwa vijana wengi wanatumia muda mwingi kucheza 'pool table' bila kufanya kazi na hivyo kupaisha kaulimbiu ya 'Hapa Kazi Tu'.

Hapo akasisitiza hoja zenye kaulimbiu hiyo, akitumia vifungu vya kiimani, mathalani 'asiyefanya kazi na asile,' akihimiza kila mtu kufanya kazi na ale kwa jasho lake. Kufanya kazi si kukaa tu chakula kije mezani, ila ni kutoa jasho kwa mujibu wa imani ya Dk. JPM.

Enzi hizo polisi wakahamia baa kusaka wanaokiuka utaratibu huo, watu wakikamatwa na wengine kutozwa faini, wapo waliowekwa ndani na kutolewa baadaye.

Sababu na hoja kuu inayohimizwa muda wa kukaa baa uheshimiwe, ambao uko kisheria ili watu wafanye kazi. Hebu fikiria, kisa cha mstaafu aliyekutwa baa akakumbwa, na mfanyakazi aliyekuwa usiku na mchana akijipumzisha baa na kinywaji chake, naye akanasa.

Vilevile mfanyakazi aliyekuwa likizo na akaamua kwa kipato chake kujiburudisha baa, naye alizongwa!

Huku na huko, wenye baa wakaona isiwe shida, watalipa nini wafanyakazi, watalipiaje umeme, watalipiaje maji, watalipaje kodi? Wakapunguza wafanyakazi na wengine wakageuza baa kuwa shule za chekechea. Ya nini mateso?

Mauzo yakashuka hata kuzamisha mapato ya pande nyingi, ikiwamo serikalini. Kukaibuka wazo, nini kifanyike?

Leo hii, Dk. Magufuli keshatangulia mbele za haki. Umma tuliobaki, nasi tunaendelea kushuhudia bajeti ya mwaka. Sura mpya, haigusi sana maeneo ya kinywaji.

Tunasikia mikoani baadhi ya wakuu wanahanikiza kwanini watu 'wasile bata' saa 24 au kwanini maduka yasifunguliwe saa 24? Hoja ni mtu ana kipato chake, ana kazi yake anakunywa pesa yake, inakuwaje?

Leo hii, tunasikia kwenye bajeti yetu kodi imepunguzwa kwenye michezo ya kubahatisha, ili vijana 'wabeti' zaidi na pesa iingie kwenye sanduku la pesa za taifa. Yahusuyo mabadiliko hatuko sana kwenye pombe, tumehamia kwenye kamari na bahati nasibu!

Leo, kila kituo cha redio kinachezesha bahati nasibu na kuangaliwa washindi ni walalahoi. Ni nani wamiliki wa vituo hivi vya kubeti? Alamsiki!

UCHUMI

# Chuo cha Baharia chaamua kujikita kuendana na uchumi wa bluu nchini

## •Mkakati mpya kunoa mabaharia uvuvi
## •Maboresho yaja, upanuzi mkoa Pwani

**Na Mwandishi Wetu**



Kaimu Mkuu wa Chuo cha Bahari, Tumaini Gurumo, akizungumza na waandishi kuhusu uchumi wa bluu. Kulia kwake ni Makamu Mkuu wa chuo (Utawala), Dk. Lucas Pastory na kushoto, ni Makamu Mkuu wa chuo hicho, (Fedha) Jonson Kileo . **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

HIVI karibuni Chuo cha Baharia (DMI), kiliandaa kongamano kujadili uchumi wa bluu kwa ajili ya kuibua fursa zilizoko baharini na namna zinavyoweza kusaidia kuinua uchumi wa nchi.

Uchumi wa bluu, ni dhana mpya inayozungumzia namna Watanzania wanavyoweza kunufaika na rasilimali za kiuchumi zinazopatikana baharini, kinyume na fikra za kuishia upatikanaji samaki pekee.

Baadhi ya rasilimali zinazozungumzwa kwenye uchumi wa bluu, ni pamoja na samaki na viumbe vinavyopatikana baharini, visiwa vilivyomo, meli za uvuvi, kilimo cha mwani, utalii na mazao mengine ya bahari.

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Muungano, zimeamua kulipa uzito mkubwa suala hilo la uchumi wa bluu, kutengeneza mazingira ya kuwanufaisha Watanzania wote.

Kwenye mkutano wa hivi karibuni jijini Dra es Salaam, Waziri wa Uchumi wa Bluu Zanzibar, Suleiman Makame, anasema Watanzania hawajanufaika ipasavyo na fursa zilizopo na badala yake wageni ndio wamekuwa wakinufaika nazo.

Anatoa mfano, meli za kigeni zimekuwa zikivua samaki wengi kwenye bahari kuu, zikichukua rasilimali hizo ambazo zingeweza kuwanufaisha Watanzania waondokane na maisha duni.

Waziri Makame anasema, Watanzania wengi wanafanya uvuvi wa kujikimu tu, usiowasaidia kuondokana na maisha duni, huku wageni wakiendelea kutumia fursa hizo kuchukua samaki na viumbe wengi kwenye bahari kuu.

Ili kuikabili hali hiyo, anafafanua kwamba hivi sasa serikali inaweka mazingira bora kuhakikisha kipaumbele kwenye fursa zilizoko kwenye uchumi wa bluu kinakuwa kwa Watanzania, kabla ya wageni kuzifikia.

Makame anasisitiza haja ya baadhi ya Watanzania ambao wameonyesha kuchangamkia na kuzitumia kwa uzalishaji fedha, zitakazopatikana hata kuwasaidia kwa maendeleo, hata hivyo wakibaki wengi kwenye mzunguko wa uchumi, kuwa zaidi wageni.

"Kwa muda mrefu tumeona meli za uvuvi za kigeni zikivua kwenye bahari yetu, zikichukua rasilimali zetu zilizopo baharini na sisi kubaki kuwa watazamaji. Mimi nadhani huu ni wakati wa kujipanga, ili tuzitumie wenyewe kwa sababu uwezo huo tunao," anafafanua.

Pia, Waziri Makame anaeleza kwamba suala la kuwapo maharamia kwenye bahari kuu wanaojitokeza kwa wingi kuchukua rasilimali za nchi, lisitishwe, ibaki kwa wananchi kudumu kuvua kwenye bahari kuu.

Kwa mujibu wa Makame, hadi sasa serikali inaweka mazingira mazuri kuhakikisha kuna kipaumbele kwa Watanzania kushikilia uchumi wa bluu, kabla ya wageni.

Anashauri, iwapo Watanzania wengi watachangamkia fursa hizo na kuzitumia kwa uzalishaji fedha, zitakazopatikana zitawasaidia kuwaendeleza na wabaki kwenye mzunguko wa uchumi, tofauti na fursa hizo zikiwa kwa wageni.

"Kwa muda mrefu tumeona meli za uvuvi za kigeni zikivua kwenye bahari yetu zikichukua rasilimali zetu zilizopo baharini na sisi kubaki kuwa watazamaji mimi nadhani huu ni wakati wa kujipanga ili tuzitumie wenyewe kwa sababu uwezo huo tunao," anasema

Anasema kwenye bahari kuu, kuna maharamia wamekuwa wakijitokeza kwa wingi na kuchukua rasilimali za nchi, hali ambayo siyo sahihi.

Waziri anasema, Watanzania wengi bado hawajaitumia bahari ipasavyo, kwa kuendelea kufanya uvuvi mdogo, hivyo kuna haja ya kubadilika wakaenda kuvua kwenye bahari kuu, ili kuchangia kwenye kukuza uchumi, kwani ndiko wanakopatikana samaki wengi.

"Sisi Zanzibar tumeshaanza kujipanga kwenda kwenye uvuvi wa bahari kuu na nyinyi mjipange msiendelee kuwa watu wa kutoa vibali vya uvuvi kwa wageni na kubaki kuwa wasindikizaji wakati rasilimali zinazidi kuchukuliwa na wageni, tubadilike kama tulivyobadilika kwenye madini," anasisitiza Waziri.

Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), Dk. Tumaini Gurumo, anasema ni muda mrefu sasa Watanzania wengi wamekuwa wakifanya uvuvi mdogo wa kujikimu na usiokuwa na tija.

Katika hilo, anasema dhana iliyoko sasa ya uchumi wa bluu, ni kwamba serikali inawataka wananchi wabadilike, hata kuachana na uvuvi wa kujikimu na waende bahari kuu.

"Kuna watu wanaishi kando ya maji, lakini wamezoea uvuvi wa mlo wa siku unakuta mtu amezoea akiamka asubuhi, babu yangu alikuwa anaenda kuchukua samaki kidogo hapo kusogeza maisha, sasa hayo tunataka kuachana nayo twende mbali zaidi," anasema Dk.Tumaini

Kuhusu mafunzo ya mabaharia, Dk. Tumaini anasema kwa mwaka chuo hicho kinazalisha mabaharia 100 wanaokidhi soko la ndani na wengine wa kufanya kazi nje ya nchi.

"Soko la mabaharia ni kubwa sana. Sisi tunazalisha 100 kwa mwaka ambao wanakidhi mahitaji ya ndani na wengine wanakwenda kufanya kazi nje ya nchi. Vijana wachangamkie fursa hii, kwa sababu ina fedha za kutosha na ajira yake siyo ya kuhangaika," anasema Dk. Tumaini

Anafafanua, DMI inajipanga kuanza kufundisha mabaharia wa uvuvi kutokana na changamoto iliyotolewa na Waziri wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi Zanzibar, Suleiman Makame.

Waziri huyo, anasema kuna mabaharia wengi, lakini siyo wa uvuvi, hivyo anakielekeza chuo hicho kuhakikisha kinaweka kwenye mitaala yake mafunzo kwa mabaharia wa uvuvi, kwa sababu utaalamu wao unahitajika kwenye meli za uvuvi ambazo serikali inatarajia kuzinunua.

**CHUO KUSUKWA**

Hadi sasa chuo pekee kinachofundisha fani ya ubaharia nchini ni DMI na hadi sasa kiko katika hali ya uchakavu wa miundombinu yake, huku serikali ikiahidi kuboresha miundombinu hiyo kwa kukipa vifaa vya kisasa, ili kiwe na viwango vya kimataifa.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, anasema eneo kilipo Posta, Dar es Salaam ni dogo, hivyo serikali inaangalia uwezekano wa kutenga eneo kubwa mkoani Pwani kwa ajili ya kukifanyia upanuzi.

Anasema kwa kuanza, serikali imeshatenga Sh. bilioni moja kwa ajili ya ununuzi wa mfumo wa kufundishia ma nahodha wa meli inayofahamika kama 'Stimulators.'

Anafafanua: "Niliwahi kutembelea hiki chuo hivi karibuni na kwa kweli nilijionea mwenyewe miundombinu ilivyo chakavu, lakini mkakati uliopo ni kukiwezesha kuwa cha kisasa na kitakuwa na majengo yenye viwango na kwa kuwa wana maeneo makubwa mkoa wa Pwani, itakuwa kazi rahisi kwetu."

Mwenyekiti wa Bodi ya DMI, Kapteni Ernest Bupamba, anaiomba serikali iliangalie kwa mtazamo wa kina, kwani ndicho chuo pekee kinachotoa mafunzo ya bahari nchini na kuzalisha wataalamu



Watumishi wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), katika hafla mojawapo ya Siku ya Wafanyakazi Duniani. **PICHA: DMI.**





## TAMISEMI yashtukia dosari maoteo bidhaa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imeagiza Timu za Usimamizi wa Huduma za Afya Ngazi ya Mkoa(RHMT) na za Halmashauri (CHMT) kujadili taarifa za maoteo ya bidhaa za afya kabla ya kuwasilishwa wizarani kutokana na kubainika dosari mbalimbali.

Dosari hizo ni pamoja na baadhi ya bidhaa za afya kutofanyiwa maoteo, takwimu kutoendana na uhalisia na halmashauri zingine kuomba mashine za maabara zenye uwezo wa kutumika Hospitali za Kanda na Taifa tu.

Mkurugenzi Msaidizi wa Afya wa Ofisi hiyo, Dk. Paul Chaote, alitoa kauli hiyo juzi kwenye kikao kazi cha Wafamasia na Waratibu wa Huduma za Maabara wa Mikoa nchini kilichoandaliwa na TAMISEMI kwa kushirikiana na mashirika yanayojishughulisha na masuala ya afya ambayo ni Global Health Supply Chain na Tanzania Health Promotion Support (THPS).

Alisema kwa mwaka wa fedha 2019/20, walianza utaratibu wa maoteo ya bidhaa hizo kuanzia vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya msingi na taifa na kubaini dosari hizo.

"Hili limenisikitisha sana kuona hali ya uwajibikaji unapungua kwenye masuala muhimu ya kitaifa, sasa ninaagiza CHMT na RHMY kuwa na utaratibu wa kujadili taarifa za maoteo," alisisitiza.

Alihimiza timu hizo kufanya usimamizi shirikishi kwa vituo vya kutolea huduma za afya mara kwa mara wenye tija na matokeo chanya.

Pamoja na hayo, aliwaagiza wafamasia na wataalamu wa maabara kuhakikisha zana za usimamizi na ufuatiliaji wa bidhaa za afya zinakuwapo mahali husika na zijazwe kila siku.

"Nyie ndio wataalamu wenye dhamana na mnyororo wa ugavi wa bidhaa za afya, mhakikishe ukaguzi wa bidhaa za afya unafanyika kila robo mwaka na kutuma taarifa Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuonyesha hatua zilizochukuliwa kwa yale yote yaliyobainika," alisema.

Msajili wa Bodi ya Maabara Binafsi, Dominic Fwiling'afu, alisema Watanzania wana tabia ya kutumia dawa bila kupima na kuwataka wataalamu hao kusimamia majukumu yao kwa weledi.

"Tumefanya ukaguzi Dar es Salaam, hali ni mbaya, kuna maduka ya dawa yanafanya vipimo, eti yanaandika malaria plus na unapewa dawa," alionya.

Msajili wa Baraza la Famasia, Elizabeth Shekalaghe, alisema kuna maduka ya dawa yana maabara huku maabara zikiwa maduka ya dawa na kuwataka wataalamu hao kwenye mikoa kuwajibika ipasavyo ili huduma zitolewe kulingana na miongozo iliyoko.

# Serikali yagawa vishkwambi mapambano dhidi ya VVU

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imezindua ugawaji wa vishkwambi zaidi ya 4,000 kwa walimu wa shule za msingi na sekondari kwenye halmashauri 18 nchini, ili kusaidia kupunguza maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) kwa wasichana balehe na wanawake vijana.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Uratibu na Bunge, George Simbachawene, alizindua ugawaji huo juzi jijini hapo kwa niaba ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ambavyo vimetolewa na Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS) kupitia mradi wa Timiza Malengo kwa Wasichana na Wanawake Vijana.

Alisema vishikwambi hivyo vinalengwa kutumika kama nyenzo za kuwafundisha wasichana hao wenye umri wa miaka 10 hadi 24 kuhusu elimu ya VVU na Ukimwi ili kutimiza malengo yao.

"Mradi huu unalenga kuwasaidia wasichana walio ndani na nje ya shule kuwa na uwezo wa fikra, maarifa na maadili ili wakati wote wabaki salama dhidi ya maambukizi ya VVU na waweze kutumika kulijenga taifa imara," alisema.

Simbachawene alisema asilimia 68 ya nguvu kazi nchini ni vijana, hivyo kuna kila sababu ya kulilinda kundi hilo dhidi ya maambukizi hayo.

"Moja ya njia muhimu zitakazotuwezesha kudhibiti maambukizi ya VVU kwa vijana ni kwa njia ya elimu kuhusu masuala ya Ukimwi, niwapongeze TACAIDS kwa uratibu huu ili kuwajengea uwezo walimu kuelimisha vijana," alisema.

Aliwataka wakurugenzi wa halmashauri zinazotekeleza mradi huo, kusimamia kwa ufanisi utekelezaji wake ikiwamo kuanzisha klabu za Ukimwi ili wanafunzi wajadili na kujifunza mada zilizoko kwenye vifaa hivyo.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, aliwataka walimu kutunza vifaa hivyo na vitumike kwa malengo yaliyokusudiwa.

Alisema baada ya sensa, vishkwambi vilivyonunuliwa vitagaiwa kwa walimu ambapo vitabu vya kiada na ziada vitapatikana humo ili kupunguza gharama za kusambaza vitabu.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, Dk. Leonard Maboko, alisema mradi unaolenga kuhakikisha wasichana walioko shuleni, wanakaa na kutimiza malengo yao na kutojiingiza kwenye tabia hatarishi.


"Na wale waliopo mitaani ambao hawana kazi za kufanya, mradi huu unawasaidia kuwapa elimu ya ujasiriamali na kuwapa ruzuku kuanza miradi midogo ili kuhakikisha inasaidia kujikinga na VVU," alisema.

Aliongeza kuwa mradi upo kwenye mikoa mitano ya Dodoma, Singida, Tanga, Geita na Morogoro na kwamba taarifa zote ambazo walimu wanapaswa kutumia kufundisha, zipo kwenye vishkwambi.

Akitoa ufafanuzi zaidi kuhusu mradi huo, Kelvin Kisoma kutoka TACAIDS Idara ya Mwitikio wa Kitaifa, alisema unagharimu Sh. bilioni 55.2 na unafadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria (Global Fund) na unalenga kuwafikia wasichana milioni moja.

Alitaja halmashauri 18 ambazo zinatekeleza mradi huo ni Manispaa ya Morogoro, Mji wa Ifakara, Wilaya ya Mlimba, Malinyi, Ulanga, Jiji la Tanga, Wilaya za Geita, Chato, Singida na Iramba pamoja na Manispaa ya Singida.

Nyingine ni Jiji la Dodoma, Wilaya za Chamwino, Kongwa, Mpwapwa, Kondoa na Bahi pamoja na Mji wa Kondoa ambapo kila shule kwenye halmashauri hizo itapata vishkwambi viwili.




Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (kushoto), akipeana mikono na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Patrobas Katambi, wakati akimkabidhi mfano wa hundi ya thamani ya Sh. bilioni 11.85, ambayo ni gawio kutoka Benki ya CRDB, jijini Dodoma juzi. Wengine ni Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), CPA Hosea Kashimba (katikati) na viongozi wa benki, Wizara ya Fedha na PSSSF. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# UN Women yawapa mbinu wabunge usawa wa kijinsia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Uwezeshaji wa Wanawake (UN Women), limeshauri wabunge wanawake kuhakikisha kila mipango wanayoipitisha bungeni, ionyeshe inasaidiaje kijinsia ili kuinua wanawake.

Mtaalamu wa Jinsia wa UN Women, Stella Manda, alitoa rai hiyo juzi alipowasilisha mada kuhusu uingizwaji wa mambo ya jinsia bungeni kwenye semina ya Chama cha Wabunge Wanawake(TWPG) iliyoandaliwa kwa kushirikiana na shirika hilo.

"Mipango mnayopitisha, hakikisheni haiwi kimya kijinsia, ionyeshe inasaidiaje kijinsia, hata ripoti ya CAG iangalieni kwa dhana ya kijinsia, wabunge wanawake mna wajibu wa kuongeza kasi ya upendeleo ya kijinsia," alisema.

Alisema upendeleo wa wanawake usiwe kwenye uongozi pekee, bali uwe kwenye kila kitu.

"Kwa mfano, kitendo cha serikali kufuta ada kwa kidato cha tano na sita kitasaidia watoto wa kike wengi zaidi kupata elimu kwa kuwa kwa sasa wapo wachache na hiyo ilichangiwa na ukosefu wa ada," alisema.

Pia alishauri wabunge wanaume kuonyesha jamii ya wanawake upendo kama inavyowaonyesha wanawake wa familia zao.

Akichangia katika semina hiyo, Mbunge wa Moshi Vijijini (CCM), Prof. Patrick Ndakidemi, alishauri serikali iangalie namna ya somo la jinsia lifundishwe shuleni ili watoto wakue wakiwa na uelewa wa haki zao na kuheshimu wenzao.

Mbunge wa Kigamboni (CCM), Dk. Faustine Ndugulile, alishauri Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 irekebishwe na wabunge wanawake wawe mstari wa mbele kupigia debe.

Akihitimisha hoja za wabunge, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alisema serikali inaweka mikakati kila mpango wanaoufanya kuhamisha usawa wa kijinsia unaoshirikisha kwa karibu wanaume.

Alisema watawajengea uwezo maofisa ustawi wa jamii wapite vijijini kuelimisha jamii masuala ya mila potofu na ukatili wa kijinsia ili kujenga jamii yenye usawa.





# Wakulima tumbaku waanza kupata neema

Na Nebart Msokwa, CHUNYA

WAKULIMA wa tumbaku waliokuwa wanakosa mahali pa kuuza mazao yao kutokana na uhaba wa wanunuzi wameanza kupata neema baada ya kampuni mpya ya ununuzi wa zao hilo ambayo pia inamiliki kiwanda cha kuzalisha bidhaa za tumbaku kutambulishwa rasmi.

Kampuni hiyo mpya, Amy Holding Company Limited imeshakinunua kiwanda cha Morogoro kilichokuwa kinamilikiwa na Kampuni ya TLTC ambayo ilijitoa kwenye ununuzi wa tumbaku nchini.

Ilitambulishwa juzi wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya na Mkuu wa mkoa huo, Juma Homera na kufanya kampuni zinazonunua zao hilo kuwa mbili na kuleta neema kwa wakulima kutokana na kupata bei ya ushindani.

Akizungumza wakati wa kutambulisha kampuni hiyo, mmiliki wa kampuni hiyo, Ahmed Howel, alisema lengo ilikuwa kuanza kununua tumbaku msimu ujao wa kilimo, lakini serikali ilimuomba aanze mwaka huu.

Alisema wanakusudia kukifungua kiwanda hicho mwaka huu na wanahitaji kupata kilo 10,000 za tumbaku kwa ajili ya kuanza uzalishaji baada ya kuombwa na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kukiwasha mwaka huu badala ya mwakani.

Alisema kwa kuanzia wanakusudia kununua tumbaku ambayo wakulima wamezalisha kwa ziada kulingana na malengo waliyokuwa wamekubaliana na wanunuzi waliopo na kwamba lengo lao sio kuwapora masoko wanunuzi waliopo.

Howel alisema kwa Wilaya ya Chunya, wanakusudia kuingia mkataba wa ununuzi wa tumbaku na vyama vinne vipya vya wakulima (AMCOS) ambavyo vinatarajiwa kusajiliwa hivi karibuni pamoja na kununua tumbaku yoyote itakayokuwa imebaki.

"Waziri Bashe alitutaka tukiwashe kile kiwanda ili kuwapatia wakulima wetu soko pamoja na kuzalisha ajira kwa vijana pale mkoani Morogoro, lakini kwa mwaka ujao wa kilimo tunakusudia kununua kilo milioni 30," alisema Howel.

Aliwataka wakulima waongeze uzalishaji kwa kuwa wao hawatakuwa na kiwango maalumu cha ununuzi na badala yake watanunua tumbaku yote ambayo wakulima watazalisha kwa msimu.

Akiitambulisha kampuni hiyo, Homera alisema serikali inahitaji kampuni nyingi zaidi kwa ajili ya kuongeza ushindani ili wakulima wanufaike kwa kupata bei nzuri na ya ushindani tofauti na ilipokuwa moja pekee.

Homera alisema katika maeneo mengi nchini zinaibuka kampuni za ununuzi wa tumbaku, lakini zinachukua mazao ya wakulima na kutokomea nayo bila kuwalipa hali ambayo inasababisha hasara.

Alisema baadhi ya kampuni hizo aliwahi kuzikamata viongozi wake na kuwatia ndani mpaka walipolipa na baadhi yao walishindwa kuwalipa na kusababisha serikali kutumia mbinu zingine kuwalipa wakulima.

"Wastani wa uzalishaji wa tumbaku kwa Wilaya ya Chunya ni kilo 9,000,000 mpaka milioni 10, sasa tunatakiwa kuongeza uzalishaji kwa kuongeza usajili wa vyama vya msingi na hapa naagiza hivi vyama vinne ambavyo vimeomba usajili visajiliwe ndani ya wiki moja," alisema Homera.

Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika wa wakulima wa Tumbaku wilayani Chunya (CHUTCU), Phesto Nshishi, alisema ili kuwaandaa wakulima waliamua kufanya mikutano na vyama vyote 18 vya msingi kwa ajili ya kuhamasisha uzalishaji.

Aliwataka wakulima kuhakikisha wanaingia shambani na kuzalisha kwa wingi ili kukidhi mahitaji ya masoko yote yanayohitajika kwa sasa.



Mkuu wa wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya, Mayeka Simon Mayeka (kulia), akisikiliza maelezo kutoka kwa wataalamu wa vipimo vya madini kuhusu asilimia za madini mbalimbali wakati wa kongamano la nishati na madini la mkoa huo, hivi karibuni. PICHA: NEBART MSOKWA

# Walalamikia vipimo batili viazi mviringo

Na Nebart Msokwa, MBEYA

WAKULIMA wa viazi mviringo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali kuwadhibiti wafanyabiashara wa zao hilo wanaonunua kwa kutumia vipimo visivyokuwa rasmi wakidai kuwa utaratibu huo unawanyonya.

Wakizungumza na Nipashe juzi baadhi ya wakulima hao walisema baadhi ya wanunuzi wanatumia vifungashio vikubwa ambavyo vina ujazo wa ziada.

Mmoja wa wakulima hao, Joseph Mboya, alisema wanunuzi hao wanaenda na mifuko mikubwa ambayo wanajaza viazi na kuweka mpaka ushungi hali waliyodai inawanyonya.

Alisema kwa sasa gharama za uzalishaji wa zao hilo ni kubwa na hawatakiwi kutumia vipimo hivyo ambavyo vinawaongezea hasara.

"Mwaka huu mbolea zinauzwa bei ya juu sana hivyo hawa wanunuzi wanatakiwa waje na mizani lakini sio huu utaratibu wa kuja na mifuko yao ambayo wanajaza mpaka wanaweka lumbesa," alisema Moya.

Naye Suma Jacob, alisema kwenye biashara ya zao hilo wameibuka madalali wanaowapokea wateja na kwenda nao shambani hali waliyosema inawapunguzia faida kwenye kilimo hicho.

Alisema wakati mwingine bila kupitia kwa dalali wakulima hawawezi kuuza mazao yao na kuiomba serikali kuwadhibiti madalali hao ili wakulima wauze moja kwa moja mazao kwa wateja.

# W'biashara vyuma wadaiwa kuiba alama anwani za makazi

Na Nebart Msokwa, MBEYA

BAADHI ya wafanyabiashara wa chuma chakavu nchini, wameanza kuiba alama za anwani za makazi na kuziuza kama chuma chakavu hali inayoisababishia serikali hasara ya kuzirejesha alama hizo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliyasema hayo juzi wakati wa mkutano wa wadau wa biashara ya chuma chakavu wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ulioandaliwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

Mkutano huo ulilenga kutoa elimu kuhusu Sheria ya udhibiti wa taka hatarishi ambazo zinakusanywa na kuuzwa na wafanyabiashara hao zikiwamo taka za kielektroniki.

Homera aliwataka watendaji wa NEMC kutoa elimu kwa wafanyabiashara hao ili waache tabia hiyo pamoja na uharibifu wa miundombinu mingine yakiwamo madaraja na miundombinu ya umeme.

Vilevile, aliwataka watendaji wa NEMC kuongeza wigo wa utoaji elimu kwa wananchi kuhusu utunzaji wa mazingira kwa kuwa maendeleo ya viwanda nchini yamechochea ongezeko la uzalishaji wa taka nchini.

Aliyaainisha maeneo ambayo elimu hiyo inatakiwa kutolewa zaidi kuwa ni pamoja na kwenye migodi, hoteli na maeneo ya makazi ya watu ili wananchi washiriki kulinda mazingira na kulinda afya zao.

"Nawaomba ninyi ambao mmealikwa kwenye mafunzo haya mkawe mabalozi wazuri kwa wenzenu, uzalishaji wa taka nchini umeongezeka kutokana na kukua kwa maendeleo, nchi yetu imeridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa ya mazingira na lazima tuifuate," alisema Homera.

Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira wa NEMC, Mhandisi Redempta Samwel, alisema waliamua kutoa mafunzo hayo baada ya kubaini kuwa baadhi ya wafanyabiashara hao walikuwa wanakiuka sheria.

Alisema mafunzo hayo yaliwashirikisha wafanyabiashara kutoka mikoa ya Mbeya, Songwe, Njombe na Iringa na mameneja wa vituo vya Forodha vya mipaka ya Tanzania na nchi za Malawi na Zambia.

Baadhi ya wafanyabiashara hao imediwa wanafanya shughuli hiyo bila kuwa na vibali vinavyotakiwa huku wenye vibali pia wakikiuka masharti kwa kujua ama kutokujua.

"Kisheria ni kwamba kila anayefanya biashara hii anatakiwa kuwa na leseni na kwa yule anayetaka kusafirisha zipo sheria zinazosimamia ambapo anatakiwa kuwa na kibali maalumu cha kusafirishia na vipo pia vibali vya kusafirishia ndani na nje ya nchi," alisema Redempta.

Alisema Tanzania ni miongoni mwa mataifa yaliyoridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa ya kusimamia mazingira ukiwamo wa mwaka 1989 ambao unahusu udhibiti wa usafirishaji wa taka.

Alisema kwenye mafunzo hayo waliwashirikisha watu wa vituo vya forodha kutokana na wao ndiyo wanaodhibiti usafirishaji wa taka hizo kwenye maeneo ya mipakani.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo walilalamikia utitiri wa tozo na vibali kwenye biashara hiyo wakidai kuwa hali hiyo inasababisha biashara yao kuwa ngumu.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Alex Swilla, alisema utitiri wa vibali na tozo hizo unasababisha gharama za uendeshaji kuwa kubwa na kuomba kibali kiwe kimoja pekee ambacho kitakuwa na taarifa zote muhimu.





Mkurugenzi wa Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), Sharif Ali Sharif (katikati), akizungumza na uongozi wa bodi wa Chuo cha Biashara Tanzania (CBE), uliofika ofisini kwake Maruhubi Unguja juzi, kwa ajili ya kupewa eneo la ardhi kujenga chuo hicho Zanzibar katika kijiji cha Fumba. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## SUZA kuendeleza lugha ya Kiswahili ndani, nje ya nchi

**Na Mwandishi Wetu**

CHUO Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) kimesema pamoja na jukumu kubwa la kutoa taaluma, pia kinafanya kazi ya kuendeleza lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi.

Akizungumza katika kongamano la utambulisho wa tunzo ya Sheikh Hamad ya tafsiri na uhusiano wa kimataifa, Makamu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Mohammed Makame Haji, alisema kutokana na kutambulika kwa lugha ya Kiswahili duniani kumetoa fursa ya kushiriki katika tunzo hiyo.

Alisema kuwa kupitia tunzo hiyo lugha ya Kiswahili itaendelea kuenea na kutanua wigo wa kutumiwa na kwamba ni vyema kwa Wazanzibar kuitumia fursa hiyo kwa kuwasilisha kazi zao na kuingia katika ushindani.

Prof. Haji, alisema tunzo hiyo ya tafsiri kutoka Kiarabu kwenda Kiswahili inashajihisha wataalamu wa lugha nchini kuendelea kufanya kazi zaidi na kazi zao zimeanza kuzaa matunda.

Kwa upande wake mshauri wa habari wa tunzo hiyo, kutoka nchini Qatar, Dk. Hanan Al fayadh, alisema miongoni mwa masharti ya kushiriki katika tunzo ni pamoja na kazi ya mtu husika iwe imegusa mambo ya jamii na iwe imechapishwa na kuenea kwa muda wa miaka mitano.

Tunzo ya Shekhe Hamad ya tafsiri na uhusiano wa kimataifa imeanzishwa mwaka 2015 nchini Qatar na lugha ya Kiswahili kwa mara ya kwanza itashirikishwa katika tunzo hiyo kwa kipengele cha tafsiri ya lugha hiyo kwenda Kiarabu na Kiarabu kwenda Kiswahili na mshindi atazawadiwa Dola za Kimarekani 100,000.

# CBE kujenga chuo Zanzibar mwaka huu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHUO cha Biashara Tanzania (CBE), kinatarajia kujenga majengo yake nje ya Mjini wa Zanzibar utakaogharimu Sh. bilioni 10 na utaanza mwaka wa fedha wa 2022/2023.

Uongozi wa chuo hicho ukiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo, Profesa Winester Suria Anderson, upo mjini hapa na umekutana na uongozi wa Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) na kukabidhiwa eneo hilo la ardhi kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Akizungumza katika kikao hicho cha pamoja, Mkurugenzi wa Chuo hicho, Dk. Japhet Mtaturu, alisema wanahitaji kuongeza fursa za biashara Zanzibar na kutengeneza mazingira ya kuchochea ukuaji wa kijamii na kitaalamu kupitia elimu, utafiti na ushauri wa kitaalamu katika maeneo ya kibiashara.

Alisema kutokana na kasi ya kiuchumi ni lazima kuwa na wataalamu wa kibiashara ambao watabobea na kuendeleza kasi hiyo na Zanzibar imejipanga kuwa na matukio bora ya kiuchumi hasa katika uchumi wa bluu na utalii.

"Sisi kama wataalamu tumejikita kuingia Zanzibar ili kuhakikisha tunaandaa wataalamu watakaokuwa na maono makubwa na kasi iliyowekwa ya maendeleo kwa Zanzibar," alisema.

Alisema kuanzishwa kwa chuo hicho visiwani humo kuna tija katika tathmini ya kiuchumi na kusaidia kuimarisha biashara za wajasiriamali.

Alisema kuna watu wengi wamejiajiri katika sekta binafsi ambao wanafanya biashara mbalimbali, lakini wanakwama kwa kukosa msaada wa kitaalamu, kuanzishwa chuo hicho kutasaidia kuziinua sekta binafsi kwenye maeneo ya wajasiriamali ili kukuza uchumi.

Alisema, pia chuo hicho kitachochea sekta ya utalii kupitia wageni kutoka Tanzania Bara na nje ya nchi hasa ikizingatiwa kuwa chuo hicho kinaprogramu nzuri ya viwango na vipimo inayotolewa katika ukanda wa Afrika Mashariki na kati na watu mbalimbali wanatoka nchi jirani kusoma katika chuo hicho.

"Kwa sababu Zanzibar ni mji ambao upo kitalii zaidi tunaamini kupitia programu kama hizo tutatangaza utalii na kuinua uchumi wa nchi," alisema Dk. Japhet.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa ZIPA, Sharif Ali Sharif, alifurahishwa na uamuzi wa chuo hicho kujenga tawi lake Zanzibar na watawarahisisha wananchi kupata elimu ya biashara.

Aliushauri uongozi wa chuo hicho kujitangaza zaidi ili kupata wananchi kutoka nje ya nchi ambao pia watafika Zanzibar baada ya kujenga majengo yao na kutoa huduma.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi wa chuo hicho, Profesa Anderson, alisema ni wakati muafaka wa kuwa na tawi la chuo hicho visiwani humo kwa ajili ya kuendelea kutoa huduma ya biashara na ujasiriamali.

"CBE kuingia Zanzibar kutakua na tija kubwa hasa katika biashara ikizingatiwa kuwa tuna utaalamu wa kutosha wa kutibu magonjwa yanayowakumba wajasiriamali katika biashara zao," alisema.

Aliipongeza Serikali ya Zanzibar kwa kukipatia chuo eneo la ardhi kwa ajili ya ujenzi huo kwa lengo la kuleta maendeleo katika sekta ya elimu na biashara.

# RC akiri mkoa wake kuongoza utoro wanafunzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, amekiri mkoa wake kuongoza kwa tatizo la utoro wa wanafunzi na sababu kubwa ni uelewa mdogo wa elimu kwa wananchi wa mkoa huo.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini hapo kuwa Wizara ya Elimu ilifanya utafiti nchi nzima na majibu yalibaini kuwa kuna utoro wa wanafunzi 30,000 Zanzibar nzima, Kaskazini Unguja pekee wanafunzi waliotoroka shule 11,000.

Alisema pia, umaskini umechangia tatizo hilo la utoro kwa wanafunzi na serikali ya mkoa huo inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa elimu.

"Umaskini ni chachu ya watoto kutoroka, mzazi anasema mtoto simuwezi...mimi nilifika hatua nikatoa tangazo mkoa mzima asije akarejeshwa mtoto shule kwa sababu hana sare ya shule ili kupunguza kasi ya utoro," alisema.

Alieleza kuwa mkoa huo unakabiliwa na uhaba wa madarasa ya kusomea na kuna upungufu wa wastani wa madarasa 305 na kazi ya madarasa inaendelea kupitia wadau mbalimbali na serikali.

Pia alisema mkoa huo unakabiliwa na changamoto ya migogoro ya ardhi kutokana na thamani ya ardhi kupanda na kila mmoja anadhani atauaga umaskini kupitia ardhi.

Alisema pia ardhi haijapangwa ikapimwa na kutolewa hati na ndiyo maana migogoro iliyoko ni ya umiliki na mipaka na mkoa utapoipanga, kuipima ardhi na kutoa hati kwa nchi nzima tatizo la migogoro ya ardhi linapungua.

"Kwa upande wetu kama mkoa tumekuwa tukishajihisha wenzetu Wizara ya Ardhi kuunda chombo cha kusimamia maendeleo yanayotokana na sekta ya ardhi na kupunguza migogoro ya ardhi isiyo na msingi," alisema.

Akizungumzia vyeti vya kuzaliwa na vitambulisho vya Mzanzibari, alisema atahakikisha kila mwenye haki hiyo na kutimiza vigezo anapata haki yake bila ya kudhulumiwa.

Vile vile, alisema kuna watu wengi hawana vitambulisho na kusababisha mrundikano mkubwa katika vituo vinavyotoa huduma hiyo na serikali yake inaendelea kusimamia hilo ili wananchi kupata vitambulisho na vyeti vya kuzaliwa.

Ayoub alisema hali ya ulinzi na usalama imeimarika mkoani humo na kuwapo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) kumechangia amani na usalama kuimarika.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PETER BUJIKU ISSEME** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA IST yenye usajili namba T245 DHB yenye CHASSIS NAMBA: NCP60022364. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/URA/RB/257783/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JAFFER ALLY OMARY,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari **ESCUDO** , yenye namba za usajili **T 637CKZ** Yenye Chassis namba **TD52W106044 ,** Engine namba **J20A150373** Yeyote atakayeona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .

**Polisi Taarifa : KIL/MOS/RB/255607/2022**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
IDARA YA UHAMIAJI

## OMBI LA URAIA



**FAIZ SHANOUDA MILAD MNTYAS RAIA WA SUDAN** AMBAYE PICHA YAKE IMEONESHWA HAPO JUU MWENYE PASPORT NAMBA PC SDN,P0 1440552

ANAOMBA URAIA WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWA MHESHIMIWA WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI, AMEISHI NCHI TANGU MWAKA 2016 KATIKA MIKOA YA DAR ES SALAAM NA SHINYANGA AKIJISHUGHULISHA NA BIASHARA ZAKE WILAYANI KAHAMA.

MTU YOYOTE MWENYE SABABU ZA KUPINGA MWOMBAJI ASIPEWE URAIA, ATUME TAARIFA YAKE YA MAANDISHI ILIYOSAINIWA KWA KAMISHINA JENERALI WA UHAMIAJI S.L.P 521 DAR ES SALAAM KWA KUTUMIA KUMB NA RPQA00448921A00

..................................
**K.n.y. KAMISHINA JENERALI WA UHAMIAJI**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **KAMUGISHA JOSEPHAT JOSEPH** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **KINGLION** yenye namba za usajili **MC 875 AMP** na Injini namba **KL157FM113J19896**, ambayo ilikuwa imesajiliwa kwa majina ya Kampuni ya King Lion Investment. Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/258890/2022.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi au apige simu namba **0627581885.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**OBADIA FAUSTINE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0586-0140** Kilichotolewa na baraza la mitihani la Taifa kupitia **KAISHO SECONDARY SCHOOL mwaka 2007.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**POLISI TAARIFA: MBE/MBE/RB/240488/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MATANGA RENATUS MBUSHI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya SUZUKI ESCUDO yenye usajili namba T544 ADZ yenye CHASSIS NAMBA : TD0LW215110, ENGINE NAMBA: GL6A401042. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/259042/2022**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI
KIVUKONI/KINONDONI
RUFAA YA MADAI NAMBA: 139 YA 2022
RAPHAEL WALIANA KAUNDA .................................... MRUFANI
BAINA YA
RHOBI WAMBURA GIKARO .................................... MRUFANIWA

Kwa
RHOBI WAMBURA GIKARO,
DAR ES SALAAM

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa Mrufani ameleta rufaa yake ambayo maelekezo ya rufaa yameelekezwa katika nakala za rufaa ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii ya mkoa, binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa kabla au siku ya **Tarehe 13 Mwezi Saba (7) Mwaka 2022. Saa 08:00 Asubuhi**

Kwa kuwa siku hiyo ni kutajwa kwa shauri unatakiwa kuja na vielelezo vyote vinavyohusiana na rufaa hii.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **30 Mwezi June Mwaka 2022.**

Hakimu Mkazi Mfawidhi
Mahakama ya Hakimu Mkazi Kivukoni/Kinondoni

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie*

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Russia yaongeza mashambulizi Ukraine

**KYIV,** UKRAINE

RUSSIA imeendelea na mashambulizi yake mashariki mwa Ukraine baada ya Jumuiya ya kujihami NATO kuitaja nchi hiyo kama tishio la moja kwa moja la usalama wa nchi za Ulaya.

Jumuiya hiyo ilisema inasimama kikamilifu na raia wa Ukraine katika ulinzi wa kishujaa wa nchi yao. Waziri wa mambo ya kigeni wa Uingereza Liz Truss alisema nchi yake itatoa silaha zaidi kwa Ukraine ambayo haitokuwa inapambana kujilinda yenyewe lakini pia kulinda eneo zima la Ulaya.

**RUSSIA YAONDOA WANAJESHI KISIWA CHA SNAKE**

WIZARA ya Ulinzi ya Russia, imesema imeondoa vikosi vyake katika Kisiwa cha Nyoka, kilichotekwa siku chache za kwanza za vita.

"Kama ishara ya nia njema, wanajeshi wa Russia wamekamilisha kazi kwenye Kisiwa cha Nyoka na kuondoa ngome iliyoko hapo," ilisema wizara hiyo.

Tangu kuanza kwa uvamizi wa Russia nchini Ukraine, Kisiwa hicho kilipewa hadhi muhimu.

Sehemu hiyo ya kuvutia , yenye miamba katika Bahari Nyeusi, kwa sasa imerudi katika udhibiti wa Ukraine.

**MAREKANI KUONGEZA MAJESHI YAKE KOTE ULAYA**

RAIS wa Marekani, Joe Biden, amesema ataongeza nguvu ya kijeshi kote Ulaya, baada ya Nato kukubali mabadiliko ya kimsingi katika kukabiliana na uvamizi wa Russia nchini Ukraine.

Alisema atajenga makao makuu ya jeshi ya kudumu nchini Poland, wakati meli mpya za kivita za Marekani zitaenda Uhispania, ndege za kivita nchini Uingereza na wanajeshi wa ardhini kuelekea Romania.

Biden alisema Nato inahitajika zaidi kuliko ilivyowahi kuwa.

Mkuu wa Nato Jens Stoltenberg, alisema Muungano huo una marekebisho makubwa kuwahi kufanyika tangu Vita Baridi.

Mpango huo mpya katika kukabiliana na Russia utawasambaza wanajeshi 300,000 walio tayari mwakani, kutoka kiwango cha sasa cha 40,000.

Biden aliuambia mkutano wa kilele mjini Madrid kwamba Nato "itaimarishwa katika pande zote katika kila nyanja - ardhini, angani na baharini".

Wizara ya Ulinzi ya Uingereza (MoD), ilisema inaongeza kwa kiasi kikubwa vikosi kwa ulinzi wa pamoja wa Nato, meli, ndege za kivita na vikosi vya ardhini.

Tangazo hilo la Marekani linaona kwamba inaimarisha uwepo wake katika bara zima lakini katika Ulaya ya Mashariki ambako makao makuu mapya ya Kikosi cha 5 cha Jeshi yatawekwa.

Biden alirudia ahadi ya muungano huo utalinda kila eneo lake.

"Tunamaanisha hivyo tunaposema shambulizi dhidi ya mtu mmoja ni shambulio dhidi ya wote." Alisema Biden

**RUSSIA INATAKA KUTEKA SEHEMU KUBWA YA UKRAINE**

Mashirika ya kijasusi ya Marekani, yamesema Rais wa Russia Vladimir Putin, bado anataka kuteka sehemu kubwa ya Ukraine.

Wanajeshi wa Russia wamedhoofishwa sana na mapigano, hata hivyo maofisa wa Marekani wanatathmini kuwa wana uwezo wa kupata mafanikio ya polepole katika lengo lao la kutwaa maeneo zaidi.

Mkurugenzi wa Ujasusi wa Kitaifa Avril Haines, alisema vita vinaweza kudumu kwa muda mrefu.

Haines alisema Putin bado ana malengo sawa na yale aliyoshikilia mwanzoni mwa mzozo.

**VITA VYA MUDA MREFU**

Katika maoni yake ya kwanza ya hadharani ya ujasusi, Haine alipendekeza uvamizi huo utaendelea kwa muda mrefu na kwamba taswira inabakia kuwa mbaya.

Kilichoweza kutokea zaidi kingeweza kuona vikosi vya Russia vikiendelea kushughulishwa na mzozo huo kwa muda mrefu.

"Wanajeshi wa Russuia hawana uwezekano wa kufanya operesheni nyingi kwa wakati mmoja kwa muda mrefu kama vita vinaendelea," alisema Haines. **BBC**



Wanajeshi wa Ukraine wakiondoa mabaki ya jengo la kibiashara lililolipuliwa na Russia katika eneo la Kremanchuk katika mkoa wa Poltava juzi. **PICHA: REUTERS**

# UN yaonya M23 kujichukulia kama jeshi

**GOMA,** DRC


MJUMBE maalum wa Umoja wa Mataifa katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo Bintou Keita, ameonya kuwa waasi wa kundi la M23 wameendelea kujichukulia kama jeshi la kawaida.

Keita alisema muonekano huo umefanya mashambulizi kuongezeka kati ya kundi hilo dhidi ya jeshi la Congo FARDC katika eneo la Mashariki, na huenda ikatoa kitisho kwa ujumbe wa kulinda amani wa Umoja wa Mataifa ulio na mamlaka ya kuwalinda raia.

Alihimiza Baraza la Usalama la Umoja huo kuunga mkono kikamilifu juhudi za kikanda za kujaribu kutuliza mvutano uliopo kati ya Congo na Rwanda, kuhusu kundi la M23 na makundi mengine ya waasi unaoleta hofu ya kutokea mapigano kati ya mataifa hayo jirani.

Mjumbe huyo pia amezihimiza nchi hizo mbili kuchukua nafasi ya kutatua tofauti zao katika mkutano wa kilele utakaoandaliwa hivi karibuni na Rais wa Angola Joao Lourenco mjini Luanda.

DRC inaishutumu Rwanda kuwaumga mkono waasi wa M23 jambo ambalo Rwanda imeendelea kulikanusha **DW**



# OPEC kutokubali kuongeza uzalishaji


**LONDON,** UINGEREZA

KUNDI la nchi zinazozalisha na kuuza mafuta kwa wingi duniani (OPEC) wakiongozwa na Saudi Arabia na Russia wanatarajiwa kubakia katika makubaliano yao ya awali ya kuongeza uzalishaji wa mafuta.

Makubaliano hayo yanatarajiwa kufikiwa katika mkutano ulioanza jana, huku kukiongezeka shinikizo la kuongeza zaidi uzalishaji.

Uvamizi wa Russia nchini Ukraine umeongeza wasiwasi kuhusu usambazaji wa mafuta na kusababisha bei ya nishati hiyo muhimu kupanda. Nchi hizo zilitangaza kuongeza uzalishaji wa mafuta hadi mapipa 648,000 kwa siku katika mwezi Julai na Agosti, hatua inayonuiwa kuleta unafuu kwenye uchumi wa dunia uliovurugika.

Mpaka sasa OPEC yenye wanachama 13 ilikuwa inazalisha mapipa 432,000 kwa siku. Katika miezi ya hivi karibu Marekani na watumiaji wengine wakubwa wa mafuta wamekuwa wakiomba OPEC kuongeza zaidi uzalishaji wa mafuta lakini wanachama kadhaa wameshindwa kufikia hili maana Iran,Venezuela na Russia ambao ni wanachama wanakabiliwa na vikwazo. **DW**



# MABAO 471 YAFUNGWA MSIMU 2021/2022

**Na Adam Fungamwango**

JUMLA ya mabao 471 yamefungwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu 2021/22, baada ya michezo 240 kukamilika, Yanga ikitwaa ubingwa kwa pointi 74 kama ilizozipata msimu uliopita ikishika nafasi ya pili, huku Simba ikiweka rekodi ya kukosa mikwaju mingi ya penalti.

Kwa mujibu wa takwimu zetu, kati ya mabao hayo mabao 35 yamepatikana kwa mikwaju ya penalti, huku Simba ikiwa kinara wa kukosa mikwaju ya penalti, ikishindwa kuweka kimiani mara tano.

Takwimu zinaonyesha kuwa jumla ya penalti 67 msimu huu zimepatikana, 35 zikitiwa kambani, 14 zikiota mbawa na 18 zikiokolewa au kudakwa na makipa.

Wakati Simba ikikosa penalti tano, timu zilizofuatia ni Biashara United ambayo imeshuka daraja na Geita Gold ambazo zimepoteza mikwaju miwili ya penalti.

Jumla ya kadi nyekundu 24 zimetolewa kwa wachezaji mbalimbali kutokana na utovu wa nidhamu.

Ni msimu ulioshuhudia 'hat-trick' tatu tu ambazo zimefungwa na Jeremiah Juma wa Prisons, Shiza Kichuya wa Namungo na ya tatu illiwekwa kwenye mechi ya mwisho ya Ligi Kuu na straika wa Azam FC, Idriss Mbombo, ambaye aliongoza mauaji na kuizika Biashara United kwenye kaburi la kushuka daraja, timu yake ikishinda mabao 4-1.

Wakati msimu huu mabao ya wachezaji kujifunga wenyewe ni 23, kipa wa Yanga, Djigui Diarra raia wa Mali ameongoza kwa kucheza mechi nyingi bila kuruhusu bao, akifanya hivyo mara 15, akifuatiwa na kipa mwenzake wa timu hiyo, Abutwalib Mshery, ambaye amepata 'clean sheets' 12, lakini zingine akitoka nazo kwenye timu yake ya zamani, Mtibwa Sugar.

Kipa wa Simba Aishi Manula ameshika nafasi ya tatu kufanya hivyo mara 11 msimu huu.

Straika aliyedhaniwa kuwa huenda akatwaa kiatu cha dhahabu baada ya kuanza kwa kasi mwanzoni mwa Ligi Kuu, Relliants Lusajo lakini akakomea kwenye mabao 10, yeye amekuwa kinara wa kutoa pasi za mwisho zilizozaa mabao 'assist', akifanya hivyo mara sita na kuwapiku Fiston Mayele na Djuma Shaaban wa Yanga, Pape Sakho wa Simba, na Pius Buswita wa Ruvu Shooting.



Mchezaji wa timu ya Ilala, Abdillah Boban (kushoto), akichuana na mchezaji wa timu ya Mburahati, Nuhu Seleman, wakati wa Ligi ya Soka la Ufukweni, katika Ufukwe wa Coco, Dar es Salaam, juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Geita kumfanyia jambo kubwa Mpole

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Klabu ya Geita Gold FC umempongeza mshambuliaji wao, George Mpole kwa kufanikiwa kuibuka mfungaji bora msimu huu akiwa na magoli 17 na wanatarajia kumfanyia jambo kubwa.

Akizungumza na gazeti hili jana Makamu Mwenyekiti wa Klabu hiyo, George Mbiligenda alisema Mpole amefanya kazi kubwa msimu huu na kudai nusu ya magoli waliyoyapata aliyafunga yeye.

"Mpole alikuwa anastahili kupata kiatu cha ufungaji bora kwani ameifanyia mambo makubwa timu yetu hadi tulipofika kumetokana na juhudi zake," alisema Mbiligenda.

Mwenyekiti huyo alisema wanamshukuru mshambuliaji huyo amewapa heshima kubwa japokuwa msimu huo ulikuwa na ushindani.

Alisema mafanikio yake yametokana na nidhamu aliyokuwa nayo na kudai ni mshambuliaji ambaye wametoka naye mbali tangu wakiwa bado Ligi daraja la kwanza.

Alisema wanatarajia kumfanyia jambo kubwa kutokana na mchango wake mkubwa ndani ya timu hiyo kwa lengo la kumpongeza ili apate moyo wa kufanya vizuri zaidi.

Alisema endapo kama itajitokeza Klabu kubwa ambayo inamhitaji wakakaa na kukubaliana watampa baraka zote ili afike mbali kupitia mpira.

## Timu 16 za veterani kushiriki bonanza la Sensa

**Na Renatha Msungu DODOMA**

TIMU 16 za Veterani zinatarajiwa kushiriki bonanza la Sensa Corporate Soka linalotarajiwa kuanza Julai 2 katika viwanja Kilimani vilivyopo jijini Dodoma.

Akizungumza na Waandishi wa Habari jana Mratibu wa bonanza hilo, Emmanuel Likuda alisema kila mwaka kutakuwa na bonanza liitwalo Corparate Fuse ambalo ni maalum kwa ajili ya kuwaleta wadau pamoja katika mambo ya burudani, kufahamiana,kushiriki michezo na kutangaza fursa nzuri zilizopo jiji la Dodoma.

Alifafanua kuwa mwaka huu bonanza hilo litajikita zaidi katika kutoa elimu kuhusiana na umuhimu wa sensa ambapo Julai 2 mwaka huu timu 16 zitashiriki bonanza liitwalo Sensa Corparate Soccer Bonanza League.

Likuda alisema bonanza hilo linatarajiwa kumalizika Agosti 20 mwaka huu na litafanyika katika uwanja wa Kilimani kila siku ya Jumamosi.

Likuda alisema Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Jabir Shekimweri anatarajiwa kufungua bonanza hilo ambapo michezo mbalimbali itachezwa kama kuvuta Kamba,kufukuza kuku,ambapo zawadi mbalimbali zitatolewa.

"Mwaka huu ndio tunaanza na tunataka kutoa elimu kuhusu sensa kupitia michezo tunataka watu wahesabiwe na katika hili tutahakikisha kila mtanzania anahesabiwa,"alisema Likuda.

## Domayo aishukuru Azam, asaka timu

**Na Shufaa Lyimo**

MCHEZAJI wa Klabu ya Azam FC, Frank Domayo ameushukuru Uongozi wa Klabu hiyo kutokana na ushirikiano mzuri waliouonyesha kwake, baada ya kumaliza mkataba wake wa kuichezea timu hiyo juzi.

Domayo alijiunga na Azam akitokea Yanga mwaka 2014, lakini amekuwa akisumbuliwa na majeruhi ya mara kwa mara na kulazimika kufanyiwa upasuaji uliomuweka nje ya uwanja kwa muda mrefu.

Akizungumza jijini jana, Domayo alisema mbali na uongozi pia anawashukuru wachezaji wenzake kutokana na ushirikiano waliokuwa wanampa.

"Nitakuwa sina fadhila nisipoushukuru uongozi wa Azam pamoja na wachezaji wenzangu, tulikuwa tunaishi kwa upendo na ushirikiano mkubwa," alisema Domayo.

Alisema yupo tayari kuitumikia Klabu yoyote itakayomhitaji kwa sasa kwa ajili ya kuendeleza kipaji chake.

"Mpira ni kazi yangu nipo tayari kuitumikia klabu yoyote itakayonihitaji, lakini hadi sasa bado sijapokea ofa yoyote."

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**BELLINGHAM KUUZWA**
KLABU ya Borussia Dortmund itakubali ofa ya pauni milioni 103 kumuuza mchezaji wake, Jude Bellingham ambaye amehusishwa na uhamisho wa klabu za Liverpool, Manchester United na Real Madrid ***(Bild via Mail)***

**RICHARLISON NA SPURS**
TOTTENHAM Hotspur jana ilifikia makubaliano na Everton ili kumnunua mshambuliaji wa Brazil, Richarlison. ***(Football.London)***

**LENGLET KUONDOKA BARCA**
TOTTENHAM Hotspur pia imeanza mazungumzo ya kumsajili beki wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 27, Clement Lenglet kwa mkopo kutoka Barcelona. ***(Sky Sports)***

**BREMER AGOMBEWA**
CHELSEA, Tottenham na Arsenal zitafanya mazungumzo na beki wa Torino, Gleison Bremer mwenye umri wa miaka 25 huku klabu hiyo ya serie A ikitaka pauni milioni 43 kumuuza mchezaji huyo wa Brazil. ***(90min)***

**WILLIAMS AKATALIWA**
LIVERPOOL imekataa ofa kutoka kwa Nottingham Forest ILI kumuuza beki, Neco Williams mwenye umri wa miaka 21, huku klabu hiyo ya Anfield ikitaka kitita cha pauni milioni 15 kumuuza mchezaji huyo wa Wales. ***(Mail)***

**DANJUMA HUYO WEST HAM**
WEST HAM iko tayari kutumia kifungu cha pauni milioni 34 ili kumsajili mchezaji wa Uholanzi, Arnaut Danjuma mwenye umri wa miaka 25 kutoka Villarreal. ***(Todofichajes)***

**PICKFORD ANUKIA EVERTON**
EVERTON iko tayari kwa mazungumzo ya muda mrefu na kipa wa England, Jordan Pickford mwenye umri wa miaka 28, ambaye amesalia na miaka miwili katika mkataba wake. ***(Guardian)***

**ARSENAL NA MARTINEZ**
ARSENAL wamewasilisha ombi la tatu la kutaka kumnunua beki wa Ajax na Argentina, Lisandro Martinez mwenye umri wa miaka 24, ambaye ana thamani ya pauni milioni 43. ***(Sun)***

**MARTINEZ AWANIWA**
KLABU ya Manchester United pia inajiandaa kuwasilisha ombi la pauni milioni 40 kumsajili Lisandro Martinez, ambaye aliwahi kuwa mchezaji wa kocha wa sasa wa mashetani hao wekundu, Erik ten Hag msimu uliopita. ***(TalkSport)***

**TIELEMANS NAYE**
KIUNGO wa kati wa Leicester City, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 25, pia analengwa na Manchester United, huku mchezaji huyo wa Ubelgiji akiingia katika kipindi cha mwisho cha mkataba wake. ***(Times)***

**COWILL NA SOUTHAMPTON**
KLABU ya Southampton inafikiria kumnunua mchezaji wa Chelsea anayechezea timu ya wachezaji wasiozidi umri wa miaka 21, Levi Cowill mwenye umri wa 19, ambaye msimu uliopita alikuwa katika klabu ya Huddersfield kwa mkopo. ***(Sun)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# LUKAKU: NAFURAHI KURUDI NYUMBANI

●●●Ni baada ya kukamilisha uhamisho wa mkopo wa muda mrefu kutua Inter Milan...

**MILAN, Italia**

ROMELU Lukaku amefichua kufurahishwa kwake na 'kurejea nyumbani', baada ya kuhitimisha kurudi Inter Milan kwa mkopo wa muda mrefu.

Lukaku aliondoka Nerazzurri na kujiunga na Chelsea kwa uhamisho wa karibu pauni milioni 100 msimu uliopita wa joto na alistahimili msimu mgumu wa 2021/22 pale Stamford Bridge.

Licha ya kumaliza kama mfungaji bora wa Chelsea akiwa na mabao 15 aliwakasirisha mashabiki kwa mahojiano yenye utata ambapo alieleza mapenzi yake kwa Inter.

Sasa, Lukaku hatimaye amepata matakwa yake na kurejea San Siro, huku klabu hizo mbili zikithibitisha makubaliano hayo kufikiwa Jumatano.

"Ni hisia za kushangaza. Tulichofanikisha hapa mwaka mmoja uliopita kilikuwa cha kustaajabisha. Hilo linafaa kwa timu, mashabiki na pia mimi binafsi," alisema katika mahojiano yaliyotumwa kwenye chaneli ya Inter ya YouTube.

"Inter imenipa mengi na ninatumaini kufanya vyema zaidi wakati huu. Sasa ni wakati wa kufanya kazi kwa bidii kama kikosi na tunatumaini kuwa bora zaidi kuliko hapo awali."

Rais wa Inter, Steven Zhang alichangia kwa kiasi kikubwa katika kumrejesha Lukaku kwa klabu hiyo kwa mkopo na Mbelgiji huyo mwenye umri wa miaka 29 alitoa pongezi za kumsifia kwenye mahojiano yake.

"Tulizungumza mambo mengi sana na jinsi ilivyokuwa haiwezekani kwangu kurudi hapa, lakini tulifanikiwa na nashukuru kwa jinsi alivyokuwa akisukuma na kuamini kuwa inawezekana.

"Tulifanikiwa kufanya hivyo mwishoni na nimefurahi kurejea.

"Ni kama kurudi nyumbani. Mimi na familia yangu tulifurahi sana hapa, shukrani kwa watu, mashabiki na wachezaji wenzangu. Tangu siku ya kwanza nilipofika hapa, kila mtu alinisaidia kutulia.

"Niliweka nyumba yangu hapa nilipoenda England kwa hivyo inamaanisha kitu."

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,010,68
MECHI KALI
BOHEMIANS FC
VERSUS
DERRY CITY
1 | 3.69
X | 3.40
2 | 1.87
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# R. KELLY AHUKUMIWA MIAKA 30 JELA

**NEW YORK, Marekani**

MWIMBAJI wa muziki wa R&B wa Marekani Robert Kelly (R. Kelly) amehukumiwa kifungo cha miaka 30 jela kwa kutumia hadhi yake kuwadhalilisha kingono watoto na wanawake.

Mnamo Septemba, mahakama ya New York ilimtia hatiani msanii huyo mwenye umri wa miaka 55, kwa makosa ya ulanguzi na biashara ya ngono.

Mzaliwa huyo wa Chicago - ambaye jina lake halisi ni Robert Sylvester Kelly - pia alipigwa faini ya dola 100,000.

Kwa sasa anakabiliwa na mashtaka tofauti ya uhalifu katika kesi nyingine tatu.

Kelly anayejulikana kwa nyimbo maarufu kama I Believe I Can Fly na Ignition - alipatikana kuwa alitumia hali yake ya umaarufu na nyanja ya ushawishi kuwavutia wanawake na watoto katika unyanyasaji wa kijinsia kwa zaidi ya miongo miwili.

Katika hukumu yake Jumatano, Jaji wa Mahakama ya Wilaya jijini New York, Ann Donnelly, alisema mtu mashuhuri alitumia ngono kama silaha, na kuwalazimisha waathiriwa wake kufanya mambo yasiyoweza kuelezeka na kuwaambukiza na magonjwa yasiyotibika.

Adhabu hiyo, alisema, itakuwa kama kizuizi dhidi ya kufanya uhalifu kama huo katika siku zijazo.

Majaji katika kesi ya Kelly ya wiki sita huko Brooklyn walisikia jinsi alivyosafirisha wanawake kati ya majimbo tofauti ya Marekani, akisaidiwa na mameneja, walinzi na wanachama wengine wa msafara wake.

Mahakama pia ilisikiliza jinsi Kelly alivyopata hati za ndoa na mwimbaji Aaliyah kinyume cha sheria alipokuwa na umri wa miaka 15 mwaka wa 1994, miaka saba kabla ya mwimbaji huyo kufariki dunia katika ajali ya ndege.

Cheti hicho, kilichovuja wakati huo, kiliorodhesha umri wa Aaliyah kuwa ni miaka 18. Ndoa hiyo ilibatilishwa miezi kadhaa baadaye.

Waendesha mashtaka wa serikali walikuwa wamependekeza kwamba Kelly ahukumiwe kifungo cha zaidi ya miaka 25, kutokana na uzito wa uhalifu wake na "haja ya kulinda umma dhidi ya uhalifu zaidi".

Lakini mawakili wake walitaka kifungo cha miaka 10 kiwango cha chini cha lazima kwa kuhukumiwa kwake au chini ya hapo.

Walionyesha Kelly kama aliyekuwa katika hali ya umaskini katika maisha yaliyojaa unyanyasaji wa nyumbani na kuteswa kuanzia akiwa na umri mdogo.

# Pogba akaribia kutua Juventus

**TURIN, Italia**

MKURUGENZI Mtendaji wa Juventus, Maurizio Arrivabene, amefichua kwamba, kurejea kwa Paul Pogba hapoTurin kunazidi kukaribia, huku mazungumzo ya uhamisho huru yakikaribia kukamilika.

Pogba aliondoka Manchester United mwishoni mwa msimu wa 2021/22 kabla ya kumalizika kwa mkataba wake, na 90min inaelewa kuwa amekubali kusaini mkataba wa miaka minne katika klabu hiyo aliyoiacha na kwenda Old Trafford mwaka 2016.

Bado kuna baadhi ya maelezo ambayo yanahitaji kutatuliwa kabla ya mkataba kukamilika, ikiwa ni pamoja na haki za picha na vipengele vingine vya kibiashara.

Hata hivyo, akizungumza na Tuttosport, Mkurugenzi Mtendaji wa Juventus, Arrivabene alifichua kuwa mazungumzo yalikuwa yakiendelea 'vizuri sana' na uhamishaji wa bure unapaswa kukamilika mapema Julai hii.

"Tunazungumza naye, mambo yanaendelea vizuri sana," alisema Arrivabene.

"Uwepo wake (Pogba) pia utakuwa wa msingi kutoka kwa mtazamo wa kibiashara, hata kama ndoto yangu ni kuwa na mchezaji wa Kiitaliano ambaye anatambulika kimataifa kama Totti, Del Piero, Buffon."



89,585/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 2.7.2022 | 22:00 | Ituano SP vs Criciuma SC | 2.41 | 2.93 | 3.18 |
| 2.7.2022 | 22:30 | Fluminense vs Corinthians | 2.23 | 3.04 | 3.48 |
| 3.7.2022 | 01:00 | Santos vs Flamengo | 2.84 | 3.14 | 2.54 |
| 3.7.2022 | 01:00 | Ceara CE vs Internacional | 2.49 | 3.04 | 2.99 |
| 3.7.2022 | 02:30 | Toronto vs Seattle Sounders | 2.65 | 3.75 | 2.43 |
| 3.7.2022 | 02:30 | CRB AL vs Guarani SP | 2.39 | 2.82 | 3.37 |
| 3.7.2022 | 02:30 | Gimnasia y Esgrima vs Defensa Justicia | 2.27 | 3.39 | 3.19 |
| 3.7.2022 | 13:30 | Suwon Samsung vs Incheon Utd | 2.49 | 3.19 | 2.89 |
| 3.7.2022 | 16:00 | Varbergs Bois vs IFK Varnamo | 2.49 | 3.15 | 2.90 |
| 3.7.2022 | 16:00 | Djurgardens IF vs Hammarby | 2.23 | 3.42 | 3.08 |
| 3.7.2022 | 18:00 | Danubio FC vs River Plate (URU) | 2.52 | 3.16 | 2.81 |
| 3.7.2022 | 18:30 | BK Hacken vs Elfsborg | 2.41 | 3.52 | 2.73 |
| 3.7.2022 | 19:00 | Union Santa Fe vs Lanus | 2.25 | 3.20 | 3.30 |
| 3.7.2022 | 19:00 | Aalesunds vs Stromsgodset | 2.24 | 3.47 | 3.02 |
| 3.7.2022 | 21:00 | Barracas Central vs San Lorenzo | 2.90 | 3.15 | 2.50 |
| 3.7.2022 | 22:00 | Atletico GO vs Sao Paulo | 2.99 | 3.04 | 2.48 |
| 3.7.2022 | 22:00 | Bahia BA vs Gremio | 2.63 | 2.78 | 3.03 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 01/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:00 | 2323 | Manly Utd vs Marconi Stallion | 2.42 | 3.49 | 2.50 |
| 12:30 | 2780 | Wollongong Utd vs Rockdale City | 2.51 | 3.59 | 2.36 |
| 13:00 | 1451 | Olympia FC vs Kingborough Lions | 8.26 | 6.29 | 1.22 |
| 13:00 | 1774 | Green Gully vs Bentleigh Greens | 2.04 | 3.49 | 3.10 |
| 13:00 | 2066 | Saif SC vs Dhaka Abahani | 2.90 | 3.40 | 2.25 |
| 13:00 | 4668 | Daejeon Korail vs Yangju Citizen FC | 1.88 | 3.19 | 3.93 |
| 13:00 | 5365 | Abahani Ltd. Chittagong vs Sheikh Jamal | 2.37 | 3.19 | 2.75 |
| 13:15 | 1531 | Gold Coast United vs Logan Lightning | 1.53 | 4.52 | 4.42 |
| 13:30 | 2123 | Souths United W vs Eastern Suburbs FC W | 3.25 | 4.30 | 1.84 |
| 13:30 | 4767 | Oakleigh Cannons vs Dandenong City SC | 1.21 | 5.90 | 9.64 |
| 14:30 | 2342 | Perth Glory Youth vs Stirling Lions | 3.24 | 3.64 | 1.94 |
| 16:00 | 5881 | Terengganu FC 2 vs Kuching FA | 1.90 | 3.48 | 3.48 |
| 16:00 | 5889 | Racing Club Reserve vs CA Sarmiento de Junin | 2.00 | 3.28 | 3.38 |
| 16:00 | 5951 | CA Platense vs Independiente Reserve | 2.60 | 3.18 | 2.50 |
| 17:00 | 1420 | Argentinos Juniors Reserve vs CA Central Cordoba SE Reserve | 1.56 | 3.90 | 5.60 |
| 17:00 | 2702 | Gareji vs FC Spaeri | 3.04 | 3.24 | 2.16 |
| 17:00 | 2994 | FC Norchi Dinamo Tbilisi vs Shukura | 3.58 | 3.58 | 1.85 |
| 17:00 | 3158 | Defensa Y Justicia Reserve vs Gimnasia de la Plata Reserve | 2.18 | 3.30 | 2.95 |
| 18:00 | 1963 | Shabab Al Ordun vs Sahab Club | 2.19 | 3.04 | 3.19 |
| 18:00 | 4793 | FK Arys vs Tobol Kostanay | 3.14 | 3.19 | 2.14 |
| 18:00 | 5172 | Otmk Olmaliq vs Navbahor Namangan | 2.11 | 2.95 | 3.49 |
| 18:00 | 5904 | FK Liepaja vs FC Riga | 3.43 | 3.43 | 1.93 |
| 18:30 | 3228 | FC KTP vs MP Mikkeli | 1.78 | 3.78 | 3.68 |
| 18:30 | 3241 | IF Gnistan vs KPV Kokkola | 2.03 | 3.58 | 3.04 |
| 18:30 | 4075 | Japs vs TPS Turku | 5.67 | 4.30 | 1.45 |
| 19:00 | 1951 | Slavia Mozyr vs Shakhter Soligorsk | 6.87 | 4.32 | 1.38 |
| 19:00 | 2643 | FM Auska Alytaus vs Kedainiai Nevezis | 1.96 | 3.44 | 3.34 |
| 19:00 | 3992 | Zalgiris vs FC Hegelmann Litauen Kaunas | 1.55 | 3.77 | 5.29 |
| 19:00 | 4461 | Kiffen vs Lahden Reipas | 3.39 | 3.73 | 1.86 |
| 19:00 | 4667 | FC Neptunas Klaipeda vs FK Babrungas Plunge | 1.61 | 4.10 | 4.60 |
| 20:00 | 1106 | Nizhny Novgorod vs Sochi | 4.70 | 3.82 | 1.60 |
| 20:00 | 4669 | GIF Sundsvall vs Malmo | 8.25 | 5.11 | 1.28 |
| 20:30 | 4196 | Ramtha Club vs FC Maan | 2.07 | 3.55 | 3.20 |
| 21:00 | 3991 | Israel U19 vs England U19 | 6.87 | 4.52 | 1.36 |
| 21:00 | 4945 | Djerv 1919 vs Vidar | 2.17 | 4.03 | 2.56 |
| 21:00 | 5392 | Vikingur Gota vs B36 Torshavn | 1.67 | 4.11 | 3.86 |
| 21:45 | 1037 | St Patricks vs Drogheda Utd | 1.38 | 4.32 | 6.87 |
| 21:45 | 1584 | Bohemians FC vs Derry City | 3.69 | 3.40 | 1.87 |
| 21:45 | 2607 | Galway United vs Waterford Utd | 2.36 | 3.20 | 2.75 |
| 21:45 | 3200 | Dundalk FC vs UCD Dublin | 1.22 | 5.28 | 10.76 |
| 21:45 | 4857 | Bray Wanderers vs Cork City | 5.88 | 4.02 | 1.47 |
| 21:45 | 5125 | Wexford Youths vs Athlone Town | 1.45 | 4.62 | 5.11 |
| 21:45 | 5230 | Cobh Ramblers vs Treaty United | 2.76 | 3.50 | 2.22 |
| 22:00 | 3107 | Finn Harps vs Shamrock Rovers | 7.07 | 4.32 | 1.38 |
| 22:15 | 3647 | Kordrengir vs Grotta | 1.86 | 3.87 | 3.28 |
| 22:15 | 4168 | UMF Grindavik vs UMF Selfoss | 2.02 | 3.77 | 2.94 |
| 22:15 | 4755 | Fylkir vs Afturelding | 1.46 | 4.52 | 5.11 |
| 22:15 | 5913 | KR Reykjavik vs Vikingur Reykjavik | 2.39 | 3.44 | 2.56 |
| 23:00 | 2469 | IF Vestri vs KV Vesturbaer | 1.67 | 4.03 | 3.93 |
| 23:30 | 5947 | Ayacucho vs Academia Cantolao | 1.43 | 4.33 | 5.91 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# BODI YA LIGI ZANZIBAR YAKUTANA NA KLABU

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BODI ya Ligi Zanzibar imekutana na klabu za ligi kuu za huko na za ligi daraja la kwanza Kanda ya Pemba kwa ajili ya kufanya tathmini ya pamoja kwa msimu uliopita na kuelekea msimu ujao.

Akizungumza na gazeti hili Mtendaji Mkuu wa Bodi hiyo, Hashim Salum alisema lengo kuu la kikao hicho ilikuwa ni kufanya tathmini ya pamoja na klabu ambazo ligi yake inasimamiwa na bodi hiyo.

Alisema kikao hicho kimejadili changamoto na mafanikio yaliyoonekana katika msimu uliopita pamoja na kujadili mipango ya msimu ujao.

Alisema katika kikao hicho yapo maoni ambayo yametolewa kuhusu masuala ya kanuni na bodi hiyo imeahidi watayapeleka kwenye Kamati ya Mashindano ili kufanyiwa kazi kwa ajili ya msimu mpya.

"Kikao kimeenda vizuri japo ni cha ndani, lakini kwa asilimia kubwa tumefanikiwa," alisema.

Aliongeza; "Klabu zimetoa maoni yao ambapo mengi yamelenga zaidi kuboresha ligi yetu kuelekea msimu mpya, yale yanayohusu bodi moja kwa moja tumeyachukua na yale yanayohusu Kamati ya mashindano basi tutayapeleka huko."

Ligi Kuu ya Zanzibar katika msimu wa 2022-2023 itashirikisha jumla ya timu 16, huku daraja la kwanza itashirikisha timu 40 ambapo Kanda ya Unguja itakuwa na timu 16 na Kanda ya Pemba timu 24.



Msanii chipukizi wa muziki wa kizazi kipya, Moe akifanya vitu vyake kwenye uzinduzi wa kampeni za kuhamasisha Sensa zilizofanywa na vijana wa UVCCM mkoa wa Dar es Salaam katika viwanja vya Mwembeyanga Temeke hivi karibuni. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Geita Gold dua zote kwa Yanga

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kushika nafasi ya nne kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara timu ya Geita Gold sasa inaombea Yanga ishinde kwenye mechi ya fainali ya Kombe la FA dhidi ya Coastal Union ili kupata nafasi ya kucheza Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Geita Gold ambayo ilikuwa inaifukuzia nafasi ya tatu kwenye Ligi Kuu lakini ikapigwa kumbo na Azam FC, ikiishia nafasi ya nne na pointi zake 46, inaliangalia pambano hilo litakalochezwa kesho kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid kwa macho mawili, huku ikiomba Yanga ishinde kwani itakuwa imeikatia tiketi ya kwenda Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Kocha Mkuu Fred Felix Minziro amesema haikuwa kazi rahisi kufika hapo kutokana na mazingira ambayo walikuwa nayo mwanzo wa msimu.

"Kwanza niseme haikuwa rahisi ni kazi ngumu, mazingira ambayo nimeichukua timu wote wanayajua, namshukuru Mungu nimepambana nayo no kuongea na wachezaji, kuhakikisha wanakuwa kwenye ubora wao na wamenisikiliza, mchezaji wa ligi unatakiwa uwe vipi mpaka hivi sasa. Timu yote, wachezaji, viongozi mashabiki wana furaha kubwa kufikia hapo tulipo," alisema Minziro.

Kanuni za mashindano zinasema kuwa iwapo Coastal Union itashinda, itapata nafasi moja kwa moja ya kucheza Kombe la Shirikisho barani Afrika, lakini ikipoteza na Yanga ikapata ushindi , basi nafasi hiyo inachukuliwa na aliyeshika nafasi ya nne kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ni kwa sababu Yanga hata kama ikishinda, tayari ina tiketi yake ya kwenda kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kutwaa ubingwa.

Timu zingine ambazo zimepata nafasi ya kuiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya kimataifa ni Simba iliyoshika nafasi ya pili, na Azam FC ambayo imeshika nafasi ya tatu.

Tanzania itapeleka timu nne kwenye michuano ya kimataifa kwa mara nyingine tena.

Michezo
Ijumaa Julai 1, 2022
Nipashe



## Lukaku: Nafurahi kurudi nyumbani



Wachezaji wa Yanga, wakiwashukuru mashabiki wa timu hiyo baada ya kumaliza ligi bila kupoteza mchezo dhidi yao na Mtibwa FC juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# WAZIRI MKUU AIPONGEZA YANGA

●●●Akunwa na sherehe zake kuitangaza Tanzania, yenyewe yakanusha Mayele kuuzwa...

**Salome Kitomari, DODOMA na Adam Fungamwango, DAR**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameipongeza timu ya Yanga kwa kuibuka vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa mwaka 2021/2022.

Akitoa hoja ya kuahirisha mkutano wa saba wa bunge la 12, jana alisema kilichovutia katika shamrashamraza za ubingwa wa Yanga ni kitendo chao cha kukumbuka kuitangaza Tanzania kupitia Royal Tour nakuhamasisha ushiriki wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022.

"Hongereni sana Wananchi, mmekuwa na msimu mzuri sana na mmestahili kuibuka mabingwa,"alisema.

Aidha, alisema pia klabu ya soka ya Simba ilishaanza kuitangaza Tanzania kwenye medani za soka za kimataifa kupitia jezi zao kuandikwa Visit Tanzania.

"Niendelee kutoa wito kwa vilabu na makundi ya watanzania wanaosafiri nje kuhakikisha wanatumia jezi zetu zenye kubeba jumbe au ajenda za kitaifa kwani jukumu la kuitangaza Tanzania na ajenda zake za kitaifa ni letu sote,"alisema.

Majaliwa aliipongeza timu ya Taifa ya Wanawake chini ya miaka 17 maarufu Serengeti Girls kwa kufuzu kushiriki michuano ya Kombe la Dunia itakayofanyika Oktoba, mwaka huu, nchini India.

"Tunawatakia kila la kheri wawakilishi wetu hao ambao wataungana na Morocco na Nigeria kuiwakilisha Afrika na kukamilisha idadi ya timu 16 zitakazoshiriki fainali hizo za Dunia zikiwa ni fainali za saba tangu michuano hiyo ilipoasisiwa mwaka 2008,"alisema.

Majaliwa pia aliipongeza timu ya Taifa ya Walemavu ya Mpira wa Miguu (Tembo Warriors) kwa kufuzu kucheza Kombe la Dunia mwezi Oktoba 2022 nchini Uturuki.

"Nitoe wito kwa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kushirikiana na karibu na Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF) kuwezesha maandalizi mazuri kwa timu zote mbili kuelekea mashindano hayo ya dunia, ili tukashindane na kuitangaza vema Tanzania,"alisema.

Wakati huo huo, Yanga imekanusha taarifa zilizoanza kuenea juzi jioni mara baada ya Ligi Kuu Tanzania Bara kumalizika kuwa straika wao hatari, Fiston Meyele raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo amejiunga na Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini, huku mchezaji huyo akimpongeza George Mpole wa Geita Gold kwa kuwa mfungaji bora msimu huu.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Klabu hiyo, Senzo Mazingisa amesema jana kuwa taarifa hizo hazina ukweli wowote na Mayele ambaye amemaliza ligi akiwa wa pili kwenye orodha ya wafungaji bora ataendelea kusalia kwenye klabu hiyo mwa msimu ujao wa ligi.

"Mayele ni mchezaji wa Yanga, alisaini mkataba wa miaka miwili, bado msimu mmoja, hivyo wanachama na mashabiki wasiwe na wasiwasi. Najua hii inafanywa ili kuwavuruga Wananchi Yanga, kuna waandishi wawili wa nchini Ghana huwa wana tabia ya kutuvuruga, lakini nitawajibu," alisema Mazingisa.

Mwandishi wa habari za michezo ambaye ni maarufu mitandaoni kutoka nchini Ghana Nuhu Adams aliandika kuwa mchezaji huyo amesaini mkataba wa miaka mitatu na klabu ya Kaizer Chiefs.

Alidai kuwa Mayele alisaini mkataba wa mwaka mmoja na Yanga wenye kipengele cha kuongeza mwingine na kuongeza kuwa kwa sasa viongozi wa timu hiyo wamekuwa wakimshawishi kuongeza mkataba kwenye klabu hiyo.

Aidha straika huyo amempongeza mshindi wa kiatu cha dhahabu, Mpole ambaye amemaliza ligi akiwa na mabao 17.

## Simba wakutana kumaliza tofauti

**Na Saada Akida**

BAADA ya kupoteza ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu huu mbele ya Yanga, viongozi na wadau wa Simba wamekutana na kumaliza tofauti zao na kujipanga upya na kuweka mikakati ya msimu ujao.

Viongozi hao wanadaiwa kwamba, hawakuwa kitu kimoja kwa msimu huu na kusababisha timu hiyo kushindwa kufikia malengo ya kutetea taji la Ligi Kuu na lile la FA.

Taarifa za uhakika zilizofikia gazeti hili jana kutoka ndani ya mmoja wa kigogo ambaye hakutaka jina lake kuandikwa, alisema kikao hicho kiliongozwa na Rais wa heshima wa timu hiyo, Mohammed Dewji kwa kuzungumza mambo mbalimbali ikiwemo mikakati ya msimu ujao pamoja na kumaliza tofauti baina yao (ambazo hazikutajwa).

Alisema katika mikakati hiyo walijadili na kutathimini kikosi chao na jinsi gani ya usajili wa wachezaji wapya waliosajiliwa, lakini pia timu hiyo kwenda nchini Misri kwa ajili ya maandalizi ya msimu ujao.

**"Tulikutana kwa ajili ya kumaliza sintofahamu (hakuitaja) iliyokuwepo kwa msimu huu baada ya kushindwa kufanya vizuri na tumeweka tofaauti zetu (hakuzitaja) pembeni na sasa tumeungana upya kwa ajili ya msimu ujao na tayari tumeshaweka mikakati yetu," alisema kigogo huyo.**

Baadae mmoja wa wajumbe na wadau wa wakubwa wa Simba, Crescentius Magori aliandika ujumbe mfupi kupitia ukurasa wake wa instagram akisema: "Katika umoja wetu (kama timu) tunajenga nyumba moja, kwa sababu katika Muungano kuna nguvu ya pamoja, mazuri yanakuja."

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >